

Kanisa la Kiinjili
la Westfalia

Nilikuwa
mgeni

nanyi
mkanikaribisha

Kanisa na
Uhamiaji





**Nilikuwa
mgeni**

**nanyi
mkanikaribisha**

Kanisa na Uhamiaji

Kanisa la Kiinjili la Westfalia
Toleo kwa ajili ya Sinodi ya Novemba 2018

“Nilikuwa mgeni nanyi mkanikaribisha”
Kanisa na Uhamiaji



Kiujumla toleo hili la kuchapisha ni sehemu fupi tu ya toleo kamili. Kwa ajili ya kupata maelezo ya kina kuhusu toleo hili na nyaraka mbalimbali tafadhali tembelea tovuti yetu **kircheundmigration.ekvw.de**.

**Limetolewa na Halmashauri ya Kanisa
la Kiinjili la Westfalia**

Uongozi na wahariri:

**Aliyepanga hili toleo (Mpangilio):
Uzalishaji:**

Mawasiliano:

Altstädter Kirchplatz 5
33602 Bielefeld
Telefon/ -fax: 0521 594-0/ -129
E-Mail: landeskirchenamt@lka.ekvw.de
www.evangelisch-in-westfalen.de

Prof. Dr. Dieter Beese, Bielefeld
Carmen Damerow, Bielefeld
Dr. Jan-Dirk Döhling, Bielefeld
Prof. Dr. Traugott Jähnichen, Bochum
Dirk Johnen, Dortmund
Dr. Ulrich Möller, Bielefeld (Federführung)
Annette Muhr-Nelson, Dortmund
Christoph Lindemann, Bielefeld
wbv Media GmbH & Co. KG, Bielefeld

Tunaomba maoni yote juu ya toleo hili yatumwe kwenye ofisi kuu za Kanisa la Kiinjili la Westfalia, Carmen Damerow, Barua pepe: damerow@kircheundmigration.ekvw.de.

Tunaomba taarifa juu ya uzoefu, maelezo ya mradi na matukio yatumwe kwa Annette Muhr Nelson, Barua pepe: muhr-nelson@kircheundmigration.ekvw.de.



Dibaji

“Nilikuwa mgeni nanyi mkanikaribisha.”

Siku zote kanisa linatambua wajibu wake utokanao na neno hili. Hata Kristo mwenyewe, Muhukumu wa ulimwengu, mwisho wa nyakati hakujitofautisha na wenye njaa, wagonjwa, wafungwa na wageni. Hata sisi anatuita tuwe upande wao.

Mwaka 2015 nchi yetu, ilipokea idadi kubwa ya wakimbizi. Wengi wao wakiwa wamekimbia vita na mateso kwenye nchi zao. Wengine pia walikuja nchini mwetu wakitumaini kuwa na maisha bora zaidi kuliko makwao. Kanisa lilijuliza ni nini linaweza kufanya ili kuweza kuwasaidia hao “wageni”. Kupitia sharika, majimbo, vituo mbalimbali vya makanisa pamoja na watu wakujitolea zilitolewa huduma mbalimbali. Mfano, kuwapa malazi, mavazi, kuwafundisha lugha yetu ya kijerumani na hata kuwasindikiza kwenye ofisi za serikali.

Lakini pia wapo wakimbizi waliosaidiwa kwa kupewa hifadhi na kanisa. Licha ya hayo ni wazi kuwa kadri muda ulivyosogea na mpaka sasa zipo changamoto zinazoikumba jamii na kanisa. Lakini pia imeibuka migogoro na matatizo yanayohusiana na “wageni” hawa.

“Nilikuwa mgeni nanyi mkanikaribisha” neno hili linatutaka tusimtazame “mgeni” tu kama mtu anayehitaji msaada bali tujue kuwa “wageni” ni watu wenye utamaduni, dini na lugha ambazo ni tofauti na zetu. Wao pia hutoka kati ka mazingira yenye mitazamo tofauti ya kisiasa. Tofauti hizi zimeleta wasiwasi miongoni mwa mwenyeji na hata wageni. Tofauti hizi pia zimezaa changamoto ambazo zinatakiwa kuzingatiwa kwa kina.

Wakimbizi na wahamiaji ni watu wenye historia zao. Wao wanaweza pia kusimulia juu ya wa matatizo, mashaka na hata matumaini yao. Hawataki kutazamwa kama wapokeaji wa misaada au watu wa kuonewa huruma tu. Lakini pia hawatakiwa kutazamwa kama tishio au watu wa kuogofya.

“...nanyi mlinikaribisha”

Ili “wageni” waweze kukaribishwa ipasavyo ni lazima jamii inayowakaribisha iwe tayari kwa mabadiliko. Hivyo basi, ili kufanikisha umoja kati yetu na wao, inatubidi sisi na wao kuwa wawazi na tayari kwa mabadiliko.

Dass in den Herausforderungen der Fremdheit ChrisKatika hali ya kukabiliana na changamoto zote zinazoambatana na kuwa “mgeni” tunakutana na Kristo mwenyewe. Hii ni ahadi kubwa na changamoto vilevile.

Ndio maana ni muhimu kusikiliza na kuangalia kwa umakini ili kuweza kuona ukweli wa hali na kutambua changamoto zilizopo pamoja na kueleza wazi misimamo yetu na kuvumilia pale tunapokuwa hatuna utatuzi. Cha msingi tusiwachukulie wageni, wahamiaji na wakimbizi kama tishio au matatizo.

Kupitia “wageni”, Kristo Bwana wa Kanisa, analizawadia kanisa, kanisa lenyewe. Ufahamu huu na ahadi hii ya Bwana imefika hata kwenye Kanisa la Kiinjili la Westfalia.

Katika maeneo mbalimbali na kwa njia nyingi watu wamejenga mahusiano na “wageni” na kukusanya uzoefu wa kushangaza na wa kufurahisha pia. Hali hii inaleta matumaini. Wageni ni zawadi kutoka kwa Kristo. Kwa hiyo inatupasa kujiuliza ni yapi wakimbizi wanakuja nayo na ni mambo gani ni muhimu yafanyike ili kuimarisha amani na kuishi kwa umoja kwa kuthaminiana. Inashangaza kuona ni kwa njia gani kanisa linaweza kubadilika na hata kufunguka ili kuweza kukutana na Bwana wake “mgeni”.

Toleo hili ni mualiko wa kufikiri na kujiuliza maswali, kutoa fikra mbadala, kujadili na labda kufanya uvumbuzi wa kushangaza.

Ninawashukuru wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika kuandaa kitini hiki. Asanteni kwa jihihada, ubunifu na huduma zenu.

Nawatakia Baraka za Bwana.

Annette Kurschus

Annette Kurschus
Mwenyekiti

Yaliyomo

Dibaji	4
Utangulizi: Nilikuwa mgeni nanyi mkanikaribisha (Mathayo 25:35).....	6
“...nanyi mkanikaribisha”	6
“Nilikuwa mgeni...”	7
Kuna umuhimu gani kuzungumzia tena uhamiaji sasa?	8
1. Uhakikisho wa kibiblia/kitheolojiag	11
1.1 Ushuhuda kuhusu Uhamiaji kutoka kwenye Biblia	11
1.2 Simulizi za taifa la Israeli	13
1.3 Yesu Kristo – njiani na ugenini	16
1.4 Kanisa la Yesu katika Misioni ya Mungu	20
2. Kanisa la Yesu katika Misioni ya Mungu	22
2.1 Mchezo wa nchi wa mioyo	22
2.2 Ujerumani: Jamii yenye kujiainisha kuwa ya Uhamiaji	24
2.3 Jukumu la Dini la kuimarisha utofauti ndani ya jamii yetu	27
2.4 Njia za kuwezesha umoja na ushirikiano wa watu wenye asili tofauti	30
3. Misukumo kwa kanisa na jamii	32
3.1 Kuwa kanisa pamoja	32
3.2 Kusherekea imani kwa pamoja	36
3.3 Kuieneza na kuishuhudia imani	37
3.4 Kubeba majukumu	41
4. Matokeo yake kwa Kanisa na Jamii	45
4.1 Kuimarisha mazungumzo – Kukuza maendeleo ya kitamaduni ya kanisa	45
4.2 Kutoa hifadhi ya Kanisa – Kusisitua haki ya kupata Asylum – kuhakikisha njia salama ..	48
4.3 Kupitisha sheria ya uhamiaji	51
4.4 Kusimamia misingi muhimu	52
Hitimisho	54

Utangulizi: Nilikuwa mgeni nanyi mkanikaribisha (Mathayo 25:35)

“...nanyi mkanikaribisha”

Sentensi hii inaeleza hali ya kawaida. Mtu anayeacha makazi yake aliyoyazoea si budi akaribishwe katika makazi mapya. Hivyo watu ambao wanahama makazi yao hasa wale wanaokimbia vita kwa woga wa kuuwawa wanayo haki ya kukaribishwa. Neno hili la “nanyi mkanikaribisha” kwao humaanisha “nimenusurika kifo, nimeokolewa na nyinyi mmenipatia nafasi ya kuishi tena”. Katika hali hiyo, kukaribishwa ni jambo muhimu sana.

Haya mambo sio mgeni mfano yaliwatokea watu waliozaliwa wakati na baada wa vita kuu za dunia ambao wanaishi nchini mwetu. Baada ya mwaka 1945 watu zaidi ya milioni 12 walipoteza makazi yao na iliwabidi wakimbilie maeneo salama na kujenga makazi mapya. Kupoteza makazi si jambo dogo. Zipo namna nyingi za kupoteza makazi. Mtu huweza kupoteza makazi yake pale anapotakiwa kuikimbia nchi yake kwa sababu za kiusalama au pale nchi yake inapovamiwa au kutawaliwa na watu wageni.

Kuwafanya wakimbizi kuwa sehem ya jamii ilikuwa ni kazi kubwa iliyohitaji ushirikiano mkubwa. Kuwa na “nyumbani” au kujisikia nyumbani kuna maana nyingi mfano mtu hujisikia nyumbani pale anapokuwa na watu anaowaamini na anaishi bila uoga. Mahusiano mazuri na wale wanaokuzunguka nayo pia ni muhimu. Hakika kuwa na “nyumbani” ni baraka.

Yesu ameweka viwango vya kudumu, ambavyo vimekuwa mila zetu kama wakristo. Wale waaminio na wenye bidii wafurahie baraka za Mungu. Neno pia linasema wageni wenye njaa na kiu, walio uchi, wagonjwa na waliofungwa kwake Yesu wana mahali pa kuishi. Ni kwa baraka ya Mungu tunaweza kuishi kwa pamoja hapa duniani, zaidi ya miaka ya Edeni. Wale waishio kwa amani huishi uhalisia wa maisha ya mbinguni.

“Nilikuwa mgeni...”

Hali ya kuwa “mgeni” mahali si lazima chanzo chake kiwe ni dharula. Mfano ni ziara ambazo watu barani Ulaya hufanya katika nchi na miji ambayo ina urafiki nayo. Lakini hata urafiki baina ya makanisa rafiki ni mahusiano mema na huleta uamsho wa kipekee. Wageni wetu wanakaribishwa kama sisi tunavyopokelewa na wenyeji wetu.

Binadamu wote wana haki ya kuwa “wageni”. Hakuna mtu anayeruhusiwa kudai kuwa, wageni wasipokuwa kama sisi tusiwapokee wala kuwakaribisha. Kuwa “mgeni” na kukubaliwa havitakiwi kupishana. Hizo ni pande mbili za shilingi moja. (Fikiri, kama wanandoa wa muda mrefu wasingekuwa na tofauti zao, ndoa lazima itakosa ladha na itakuwa ya kuchosha. Fikiri dhana ya “mimi” na “wewe” isingekuepo.)

Mambo mageni huvutia pia. Mfano mzuri ni vyakula vya kigeni tunavyokula. Udadisi wetu hutufanya tuvutiwe na nchi za mbali na hivyo hutufanya tupende kusafiri. Mambo “mageni” huzoeleka na baada ya muda fulani hupoteza umaalumu wake. Ila ni muhimu kujifunza na kuthamini na kupenda mambo “mageni”.

Lakini pia ni kweli kwamba mambo mageni yanaweza kuleta wasiwasi miogoni mwa watu. Kuna msemu wa kijerumani wenye maana ya “Nchi nyingine, desturi nyingine”. Jambo geni au mambo mageni huweza kuleta wasiwasi na hata kuogopwa. Uoga huo hautokani na “ugeni” pekee, bali mazoea waliyonayo wenyeji kuanza kubadilishwa na kuonesha dalili hasi. Tutambue kuwa unaweza kumuamini mtu au kufikiri kumfahamu lakini mtu huyohuyo akakugeuka na kukusaliti kwa kutenda ukatili na uhalifu kwa watu wengine. Unaweza kumkaribisha mgeni kwako na baada ya muda akakugeuka na kuwa mtu mpenda fujo, uhalifu na misimamo mikali. Katika lugha ya Kilatini, neno “hostis” lina maana mbili: “mgeni” na “adui”. Ni muhimu kuwa makini pale tunapokutana na watu na tunapojenga mahusiano nao.

Kuna msembo wa kiafrika usemao “Kinahitajika kijiji kizima kuweza kumlea mtoto”. Kwa maana hiyo jamii inamhusisha kila mtu katika maisha ya mtoto, kwa lengo la kumuelekeza majukumu na wajibu wake katika jamii. Kwa njia hiyo kila mtu ana mchango wake kwenye jamii. Mtu anapokiuka taratibu zilizowekwa basi huwajibishwa kwa taratibu zilizopo katika jamii hiyo. Tukumbuke kwamba watu ambao wamekuja kwetu kutoka nchi nyingine wanakumbana na taratibu mpya, mfano sheria za kazi na uraia zinazowahusu wao kama wakimbizi na waomba hifadhi. Kwahiyo si ajabu watu hao, kujikuta wamekiuka taratibu na sheria. Hali hiyo ni tofauti kabisa katika makosa ya wizi, udanganyifu, mashambulizi ya aibu, unyanyasaji wa kingono na uhalifu wa kimtandao. Uhalifu huu hufanywa na wenyeji pamoja na wakimbizi na waomba hifadhi. Uhalifu huu, hauna sintofahamu. Hata wageni hao tunaowapata huko walikotoka uhalifu huo upo, wanaufahamu na kuutambua. Ni kweli kwamba kufuatia idadi ya watu kuongezeka, kupitia wakimbizi na wahamiaji, kuna ongezeko la uhalifu. Hata hivyo tafiti mbalimbali hazioneshi kuwa asilimia kubwa ya uhalifu huo hufanywa na wakimbizi au wahamiaji. Muhimu ni kwamba, lazima tutambue kuwa bila kujali asili za kitamaduni, dini na itikadi, zipo sababu ambazo zinaweza kukuza au kuzuia uhalifu..



Mwaka 2016, asilimia 22.5 ya wakazi wa Ujerumani walikuwa na asili ya uhamiaji. Kwenye jimbo la Rhein Kaskazini-Westfalia ilikuwa asimilia 27.2 (Chanzo: Kitabu cha Mwaka wa Takwimu 2017). Mtu anahesabiwa kuwa mwenye asili ya uhamiaji pale yeye mwenyewe au wazazi wake au mmoja wa wazazi wake hakuzaliwa na uraia wa Ujerumani. Raia wa kigeni/wahamiaji waliokuwa na asili ya kijerumani waliokimbia kutoka Ulaya Mashariki baada ya vita kuu ya pili na ambao kwenye miaka ya tisini walipata uraia wa Ujerumani; wote huhesabiwa kuwa na asili ya uhamiaji. Vivyo hivyo, hii inajumuisha watu ambao walizaliwa na uraia wa Ujerumani, lakini ambao angalau mzazi mmoja ni mgeni.

Kuna umuhimu gani kuzungumzia tena uhamiaji sasa?

Katika miongo iliyopita Kanisa la Kiinjili la Westfalia (EKvW), wanachama wake, sharika na taasisi zake zimekuwa zikisisitiza kuwapokea wakimbizi na kuwafanya kuwa sehemu ya jamii. Kwa kufuata misingi ya Injili, Kanisa limetoa misimamo yake juu ya masuala ya msingi na changamoto za nyakati hizi. Kwa nini leo Kanisa la Kiinjili la Westfalia linauletea umma toleo hili la “Kanisa na Uhamiaji”? Jibu letu, ni kama ilivyo kawaida katika masuala ya msingi, ni muhimu na lazima kutoa msimamo juu ya suala hili nyeti. Kwenye miaka na miezi iliyopita hali imebadilika. Matatizo yamekuwa mengi na mijadala juu ya masuala yanayohusu uhamiaji yamekua yakichukua mkondo ambao si rafiki.

Tukumbuke kuwa tangu mwaka 2015 watoto, wanawake na wanaume zaidi ya milioni moja wamekimbia vita, ugaidi, mateso ya kisiasa na ukatili kwenye nchi zao. Wamekimbilia kwetu hapa Ujerumani wakiwa na matumaini ya kuishi maisha bila uoga wa kuuwawa.

Kwa ushirikiano baina ya raia, sharika za kikanisa, taasisi binafsi, makampuni, jumuiya mbalimbali bila kusahau mamlaka za kiserikali zimefanyika jitihada na bidii kubwa kufanikisha “desturi ya ukaribishaji” wa wakimbizi na waomba hifadhi.



Nimepata marafiki wengi ambao ni wakimbizi. Nimejifunza vitu vingi kupitia mahusiano yangu na wao. Nimepokea shukurani na ukarimu kutoka kwao.

Mwanamume wa miaka 52

Hata hivyo, imeonyesha pia kuwa uhamiaji wa kasi wa idadi kubwa ya watu unaweza kuwa changamoto kubwa kwa ushirikiano na mshikamano wa jamii yetu. Matokeo yake ni wasiwasi na mvutano katika jamii. Hii ni kwakuwa suala zima la kuwafanya wakimbizi kuwa sehem ya jamii, ni gumu na huchukua muda mrefu. Lazima wajifunze lugha, hivyo wanahitaji muda, ili waelewe majukumu na nafasi zao katika jamii.

Lakini pia katika jamii, wapo watu wenye wasiwasi sana. Wasiwasi hutokana na mabadiliko yanayotokea katika jamii na dunia yetu kiujumla. Yale waliyoyazoea ghafla yanabadilika na dalili za nafasi zao katika jamii huanza kupotea. Utandawazi na mabadiliko ya kiutamaduni huwafanya kuhoji juu ya usahihi wa misingi yao ya kimaadili na kijamii kiujumla.

Kwakuwa jamii yetu inajali sana maendeleo ya “mtu binafsi”, na hivyo hufungua fursa mpya na zisizotarajiwa. Maendeleo ya mtu binafsi pamoja na mabadiliko ya ghafla, husababisha kuhoji maana halisi ya maisha. Masuala mengine yanayohojiwa sana ni usalama na mahitaji ya walio wengi. Ni vigumu kuelewa mabadiliko ya msingi yanayotokea kwa haraka katika mfumo wa uchumi wa dunia. Mwendo wa mabadiliko hayo unapunguza uwezo wa wananchi kushiriki katika mambo au maamuzi ambayo yanagusa maisha yao ya kila siku. Hali hii inaongeza hofu ya kupoteza matarajio na fursa za baadaye.

Wapo watu wengi wanao watazama wakimbizi na wahamiaji waliopo nchini mwetu kama chanzo cha matatizo. Kuwaunganisha wakimbizi na jamii sio jambo dogo, ni mchakato mrefu. Mchakato huu ni mgumu na wenye kuambatana na changamoto mbalimbali. Kuishi pamoja kama jamii yenye amani, huku kukiwa na tofauti mbalimbali za kitamaduni, dini na itikadi ni jambo zuri lakini kunaweza kutazamwa kama tishio kwa maisha yaliyozoeleka. Hali hiyo inasababisha baadhi ya wenyeji kuona wanapitwa na maendeleo na kutengwa na jamii. Wengine huwatazama wakimbizi na wahamiaji kama washindani wao kwenye soko la kazi.

Wakati huohuo tunaona jinsi wanasiasa wenye sera za kutaka umaarufu, wanavyotumia uoga wa wenyeji kujinufaisha kisiasa. Sera zao zinasambaza chuki na woga. Hasa chuki hizi zinawalenga wakimbizi na wahamiaji na wale wenye asili ya nchi nyingine. Lakini pia chuki hizi zinawalenga wale wanaopigania haki za wakimbizi na kuwasaidia. Ni lazima kuonesha msimamo dhidi ya chuki na vitisho vya namna hiyo.



Tangu mwaka 2015 nimekuwa nikiwahudumia wakimbizi. Mwanzoni kila kitu kilikuwa vizuri, nilitumia muda na nguvu zangu. Ila sasa wengine wamekuwa mzigo hasa kwa kuwa hawajui waendeleo vipi. Kuna wakati mwingine najisikia kuwa natumika kuwanufaisha wao pekee.

Mwanamke wa miaka 53

Je, kanisa linawezaje kuchangia kwenye hali hii ya kuwa na wasiwasi? Ni kwa njia gani maandiko ya kutia matumaini ya kwenye Biblia yanaweza kutumika kuwaongozo watu wenye wasiwasi? Ni kwa njia gani tumaini linalotoka kwenye Biblia linaweza kuwa chanzo cha nguvu na ushirikiano katika kutoa msaada? Maandiko yanawezaje kutupa ujasiri wa kufikiria juu ya maisha yetu ya mbeleni licha ya uwepo wa mashaka na wasiwasi?



Sina ufahamu mzuri kuhusu Biblia. Ni kweli kwamba wote wanaotajwa humu ni wahamiaji? Hili suala zima la wakimbizi na wahamiaji linapambwa pale linapohusishwa na nyakati za Yesu.

Ulrich Müller, Zimamotoa.D., Schwerte

Toleo hili la Kanisa la Kiinjili la Westfalia sio neno kutoka mbinguni bali ni mitazamo ya pamoja, yaani yetu na washirika wetu katika serikali na jamii. Tunataka kuleta uzoefu wetu na mitazamo yetu kwenye majadiliano kwenye umma. Kwa sababu sisi kama wakristo tunahitaji marekebisho, uhakikisho na ufafanuzi wa misingi yetu inayotuongoza. Hivi ndivyo tunavyoelekezwa katika kutimiza wajibu wetu kama kanisa, katika kukabiliana na changamoto hizi zinazongezeka. Kwa hiyo tutafurahi kupokea maoni yenu na kuweza kuwasiliana nanyi kupitia toleo lililowekwa kwenye tovuti yetu. Kwenye tovuti hii kirche-und-migration.ekvw.de hapa lipo toleo zima pamoja na picha, simulizi, filamu, ibada na takwimu husika).

Kubalini kutiwa moyo, tunatarajia kuona mapokeo yenu!

1. Uhakikisho wa kibiblia/ kitheolojia

1.1 Ushuhuda kuhusu Uhamiaji kutoka kwenye Biblia

Mtu yeyote anayesoma Biblia anakutana na simulizi zisizopishana sana na zile za uhamiaji unaotokea sasa. Kupitia simulizi hizi tunapata nafasi ya kulitazama suala zima la “uhamiaji” kwa jicho jingine. Uwepo wa wahamiaji unatoa fursa kwa makanisa kongwe ya Ulaya, nafasi ya kujijenga na kujipanga upya. Hata Biblia yenyewe ni kitabu kilichojaa simulizi za uhamiaji, kuanzia kitabu cha kwanza hadi cha mwisho.

Biblia imejaa habari mbalimbali kuhusu uhamiaji, mfano shuhuda za watu wa Mungu wakiwa wakimbizi. Biblia inatonesha magumu yanayoambatana na “kuwa mkimbizi” au “uhamiaji” wenyewe. Biblia pia inatonesha ujasiri, thamani, imani na baraka za wakimbizi na wahamiaji. Kwa kupitia ushuhuda huu ambapo jamii zetu ni za “uhamiaji” kanisa linakumbushwa mambo mawili ya msingi.

Moja, wakati wahamiaji wakitazamwa kama vyanzo vya matatizo, Biblia inasimulia juu ya habari ya tamaduni za kiyahudi walizotumia wao ili kukabiliana na suala la uhamiaji. Katika Biblia zipo habari za namna wahamiaji walivyotumia talanta zao kwa manufaa yao na wenyeji. Pia tunaoneshwa jinsi wao “wahamiaji” walivyokubali kuongozwa na Mungu. Biblia pia inasimulia kuhusu habari za vita, mateso na matatizo mengine yaliyowapata wahamiaji na wakimbizi.

Kwa kukumbushwa kuwa “historia ya imani” ya Biblia ni simulizi za kuhama na kuwa “mgeni” inatufanya tuwatazame wahamiaji na wakimbizi tulionao nchini kwetu kwa jicho jingine. Pili, makanisa yanapata nafasi ya kuhoji juu ya sababu zinazowafanya watu wahame makwao, au nini kinawapa watu hao ujasiri wa kuacha makazi, makanisa yao na kuwa tayari kuwa “wahamiaji” au “wakimbizi”.



Watu ukimbizini

Hadi sasa, watu milioni 68.5 duniani kote ni wakimbizi. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Bread for the World inasemekana kuwa dunia haijawahi kuwa na idadi kubwa ya wakimbizi kwa kiasi hiki. Kati ya wakimbizi kumi, tisa hukimbilia nchi zilizoendelea. Watu milioni nne wamepata hifadhi kwenye nchi maskini. Raia wengi katika nchi hizo huishi kwa chini ya dola 1.25 kwa siku.

Wingi wa simulizi juu ya uhamiaji katika Biblia

Tunaposoma Biblia tunaona habari juu ya wakimbizi na wahamiaji na hata habari juu ya vita, mapigano na migogoro kati ya mataifa na watawala wa wakati huo. Zipo habari za majeshi ya kimitisri yaliyotawala nchi na taifa la waisraeli pamoja na habari juu ya mtawala Alexanda na warumi ambao waliyavamia, kuyatawala na kuyatumikisha makabila madogo na mataifa mengine. Simulizi hizi si za amani bali za vita, vita zilizoangamiza watu wengi. Vita, kazi shokoa, utawala wa kigeni na watu kufukuzwa kwenye nchi zao ni mambo ambayo yalikuwa yakitokea kwenye falme za nyakati hizo. Uhamisho wa lazima kwa maelfu ya watu wakati wa karne ya 8 kabla ya Kristo na wakati wa karne ya 6 baada ya Kristo. Wakati huo Waebrania walilazimiswa kuhamia Babiloni. Wakati wakiwa ugenini walikutana na changamoto mbalimbali zikiwemo namna ya kuzitunza na kuziishi tamaduni zao.

Hata tunaposoma kuhusu Jakobo aliyekuwa mkimbizi au Yusufu aliyekuwa mtumwa au Esta ambaye alikuwa mhamiaji nchini Israeli tunapata kuona hali halisi ya maisha ya mataifa ya wakati huo. Maandiko hayo hayatoi tu ukweli wa wakati huo, bali ni simulizi zinazotunesha yale waliyoyaona na kuyapitia wakati huo. Lakini tunaona pia walivyomtumaini Mungu na yeye alivyojionesha kwao na kuwaongonza.

1.2 Simulizi za taifa la Israeli

Habari za kufukuzwa kutoka bustani ya Edeni (Mwanzo 3:23-24) na zile za kuondoka na kukimbia kwa Kaini kwenda nchi ya ukimbizi (Mwanzo 4: 16) zinaonesha kwamba uandishi Bibilia unahusisha historia ya wanadamu na maendeleo ya mila na ustaarabu katika jamii zilizokuwa na wahamiaji.

Historia na maisha ya wana wa Israeli na wayahudi kiujumla, ni historia ya uhamiaji. Hata mababu wa imani walikabiliana na uhamiaji walipotoka nchi zao na kuwaacha jamaa zao kuanza safari ya kuhamia nchi waliyoahidiwa, Kaanani. Mwanzo kabisa mwa simulizi hizi tunaona upekee wa taifa la Israeli: taifa teule la Mungu. Mungu anawaongoza safarini na kuwaahidi kubariki vizazi vyao (Mwanzo 12:1-4).

Somo ambalo tunalipata kupitia historia ya waisraeli ni kuwa, Mungu anatupa wajibu wa kiimani, ule wa kujiainisha pale tunapokuwa “ugenini”. Anatokumbusha umuhimu wa kujumuika na ndugu zetu. Hivyo ndivyo walivyoishi wayahudi na ndivyo wanavyoishi wahamiaji na wakimbizi tulionao nchini mwetu.

Wakati huohuo simulizi hizi zina habari za usuluhishaji wa migogoro, mipaka iliyowekwa kwa makubaliano na hata mawasiliano waliyoyafanya vizazi vya Abrahamu na wakazi wengine (Mwanzo 12-50). Watu wote walitambua uhusiano maalumu uliokuwepo kati ya kizazi teule cha Mungu na Mungu mwenyewe (Mwanzo 23: 8, tazama, 14:18), kuwa kuiona hofu ya Mungu hata pale ambapo hawakuitegemea (Mwanzo 20:14) na kwa kuitwa kwao kufanya maombi kwa ajili ya watu wengine. (Mwanzo 20:17).

Hata katika kitabu cha pili cha Musa – Kutoka tunaendelea kusoma juu ya historia ya wana wa Israeli, ambayo tunavyojua ni historia ya uhamiaji. Katiba kitabu hiki tunasoma habari za vita na mapigano habari ambazo katika kitabu cha Mwanzo hazipo. Maandiko ya Kitabu hiki pia yanaweka wazi jinsi Mungu anavyojiweka upande wa wanaoteswa na waliofanywa watumwa wa taifa la Misri. Mungu anawakomboa kutoka utumwani na kuwaweka huru. Uandishi wa torati, iliyotumika kutawala maisha ya wana wa Israeli, ulishawishika na ukombozi huo na yale waliyoyapitia na kuyaona wakiwa ukimbizini kutoka Misri.

Hata katika simulizi hizi tunaona namna makabila na mataifa mengine yalivyoivamia Kanaan, au hata wana wa Israeli yalivyopokelewa kwa chuki na makabila mengine. Tunaona taifa la Israeli linapitia mateso, unyanyasaji na ukandamizaji kutoka kwa watawala wengine.

Kuwa mgeni na Sheria

Hata katika maandiko ya torati “wageni” wana haki zao. Neno “Mgeni” katika (kiebrania “ger”) kiebrania humaanisha mtu ambaye anaishi mahali ambapo hakuzaliwa na asiyekuwa wa makabila ya sehemu hiyo. Lakini pia mtu huyo hana haki ya kumiliki mali kama wazawa wa kiume. Ndani ya torati pia tunaona taratibu ambazo wageni wanatakiwa kuzifuata. Mfano mzuri ni kuiheshimu siku ya Sabato na vigezo vingine wanavyotakiwa kuvitimize ili waweze kushiriki kwenye ibada na wana wa Isiraeli.

Torati hiyo inasisitiza mambo ambayo waisraeli wanatakiwa kuyazingatia katika mahusiano yao na wageni. Wageni wanachukuliwa kama kipimo cha mahusiano mema ndani ya jamii (Kutoka 22:20–23,9). Kwa sababu ya fursa chache walizonazo kama walivyo wajane na yatima, torati inasema watu hawa wana haki ya ulinzi maalumu dhidi ya matatizo ya kiuchumi, kisheria na kijamii. Vikundi hivi vinahakikishiwa haki ya huduma na misaada maalumu kama waliyopewa waisraeli (Kumbukumbu la Torati 14:29).

Msingi wa neno “Mpende mgeni kama nafsi yako” ni “Kwa maana ninyi (taifa la Isiraeli) mlikuwa wageni katika nchi ya Misri” (Mambo ya Walawi 19:34, Kutoka 22:20 na Kutoka 23:9).

Biblia inagusia “ugeni” kama hali ambayo haitakiwi kusahaulika, hata pale mtu anapokuwa akifurahia utajiri wa nchi yake. Kwenye hali hiyo ni muhimu kufikiria kuwa yawezekana sitakuwa mahali hapa kwa muda wote na kwa muda huu ambao nipo sipo peke yangu. Simulizi za uhamiaji hatutakiwi kuzisahau hata kama sisi wenyewe hatuguswi nazo moja kwa moja. Hata waisraeli wanakumbushwa kutosahau hali ya ukimbizi walioipitia mababu zao.

Cha kushangaza wanasahau (Kutoka 22:20). Wageni wananyayapaliwa na kunyanyasika Isiraeli (Hesabu 15:15 f.) Wageni wanatengwa na kufukuzwa Isiraeli (Nehemia 13). Wageni wanaogopwa na kuchukiwa. Lakini pia tunaona wazawa wanavyokuwa na woga na wasiwasi wa kupoteza tamaduni zao. Wasiwasi wao ni mkubwa kiasi kwamba wanaogopa ndoa kati yao na wanawake wa kigeni wakihofia kumchukiza Mungu wao (Kumbukumbu la Torati 7,23) na kupoteza “upekee” wao kama taifa la Isiraeli.

Kuhama kwa mipaka

Habari tunazo zisoma kwenye Agano la Kale juu ya mahusiano yasiyokuwa mazuri kati ya wazawa na wageni yanachukua mkondo mzuri pale tunaposoma simulizi za Ruthu na Naomi. Naomi na Ruthu wote ni wanawake wajane. Naomi anarudi kutoka ukimbizini Moabu alikopata hifadhi baada ya kukimbia njaa kali.

Naomi anarudi akiwa ametafuta wake kwa ajili ya watoto wake licha ya kuwa taratibu za wakati huo ndoa kati ya mmoabu na muisraeli ilitazamwa kuwa kinyume na mapenzi ya Mungu (tazama Ezra 9–10, Nehemia 13:23–27). Chanzo cha mtazamo huu ni simulizi juu ya wamoabu kuwanyima maji na mkate waisraeli wakati wakiwa safarini wakikatiza jangwa (Kumbukumku la Torati 23:4).

Lakini habari ya Ruthu ni habari ya aina tofauti, Ruthu ambaye ni mmoabu anaishi vizuri na Naomi, anamtunza na kumuuguza. Upendo na ukarimu wake kwa Naomi ni mkubwa mno. Ruthu kama mgeni na Naomi kama mwenyeji wanajenga uhusiano ambao unaleta faida kwa mataifa yao. (Ruthu2:10–12).

Katika mistari ya mwisho ya kitabu cha Ruthu, tunaona Ruthu anavyochaguliwa kuwa mmoja wa mabibi wa Daudi. Daudi ambaye anakuja kuhesabika kati ya wafalme mashuhuri wa Israel. Katika Agano Jipya tunaona jina la Ruthu linawekwa kwenye kitabu cha historia cha Yesu (Mathayo1:5).

1.3 Yesu Kristo – njiani na ugenini

Picha na uhalisia wa safari

Jamii za Kikristo za wakati ule na watu waliokuwa karibu na Yesu waliishi kwa kufuata Biblia. Walijua pia nini maana ya kuwa “mgeni” kama ilivyokuwa imeandikwa kwenye Biblia.

Vitabu vya Injili vinamuonesha Yesu aliyeishi kama mwanadamu hapa duniani na kama msafiri. Safari zake zinaonyesha ukaribu wa kuja kwa Mungu (Marko 1:14). Safari zake na zile za wanafunzi wake hazipishani na zile za wana wa Israeli (Mathayo 2). Ujio wa Yesu, maisha yake hadi kupaa kwake ni sehemu muhimu ya salamu zake za kuwaaga wanafunzi wake (Yohana 13–17) na sehemu ya msingi za imani ya kikristo.

Mipaka ya kikabila, kama ile kati ya watu wa Mungu wana wa Israeli na makabila mengine, iko imara na imesitizwa katika Biblia (Mathayo 10: 5). Lakini wakati huohuo, mipaka hiyo inavunjwa na Bwana Yesu (Mathayo 15: 18–21). Katika Injili, tunaona Yesu anavyokabiliana na hiyo mipaka. Hata kufufuka kwake kwa ajili ya mataifa yote ni njia mpya ya kuyaunganisha mataifa yote (Mathayo 20:28).

Kitabu cha Matendo ya Mitume kinaeleza jinsi imani inavyowafikia hata wasiokuwa Wayahudi (Mdo. 10). Wakati huohuo tunaona namna “njia mpya”, yaani kumuamini Mungu kunavyowafanya wafuasi wake Yesu kuwa wahamiaji (Mdo. 9: 2, Mdo. 11: 19–20). Wanalazimika kuyakimbia makazi yao, kwa hofu ya kuteswa (Mdo. 18: 1–3, hata Warumi 16: 3–4). Uhamiaji huo ulikuwa sehemu kubwa ya mwanzo wa kuenezwa kwa Imani ya Kikristo.

Hata kama safari ya kutoka bara la Asia hadi Ulaya, ambayo kwa sasa huitwa Uturuki hadi Ugiriki kwa usafiri wa nchi kavu haikuwa na maana kubwa kitamaduni kama wakati wa sasa lakini bado tunasoma habari za safari hii katika Biblia (Mdo.16:9–40). Tuona jinsi mitume walivyopokelewa vizuri baada ya kufika Ulaya, mji wa Filipi (Mdo. 16:11–15.40). Licha ya hilo wanakutana na Lidia, mama muuza rangi za zambarau na mcha Mungu. Lidia ambaye ni mzaliwa wa Asia ila aishie Ulaya anatuonesha kuwa hata kwa wakati ule uhamiaji ulikuwa uhalisia wa maisha kwa nyakati hizo. Kwa hiyo kuzingatia maandiko ya mitume tunaona chanzo cha Ukristo ulaya kuwa ni ukarimu wa mama mhamiaji kutoka Asia.

Makanisa machanga ya wakati huo yaliwaunganisha watu, Wahayahudi pamoja na watu wa makabila, desturi na dini tofauti. Kwa hiyo hata wakati huo watu walitafuta njia nzuri za kuishi kwa pamoja licha ya tofauti zao. Tendo hilo halikuwa rahisi, kulitokea migogoro mingi (Warumi 14, Wagalatia 2:11–14;5:1–6), mfano ni migogoro kuhusu vyakula au desturi ya tohara (1. Wakorintho 8, Mdo. 15). Miongoni mwa mafundisho yaliyozingatiwa kwa nyakati hizo, ni pamoja na mafundisho ya Paulo juu ya haki kupitia imani. Ubatizo nao unawaunganisha na kuwapatanisha watu, lakini pia ni chanzo cha usawa (Wagalatia 3:28). Maana si mipaka ya kijamii wala torati ya wayahudi inayoamua nani ni mtu wa Mungu. Maana kupitia kufa kwake Kristo na kufufuka kwake hata wasio wayahudi wanavutwa karibu na Mungu (Waefeso 2:12–19).

Kristo ndani ya wageni

“Nilikuwa mgeni nanyi mkanikaribisha” au “nilikuwa mgeni nanyi hamkunikaribisha” (Mathayo 25:35,38,43) hivyo ndivyo msimulizi anavyoandika kuhusu Yesu mwana wa Adamu, hakimu mkuu wa dunia na mfalme. Ujumbe wake uko wazi, yaani kama tunayowapokea wenye njaa, wagonjwa na waliofungwa – kwa kipimo hicho ndivyo mfalme atakavyohukumu matendo yetu na kutotenda kwetu dhidi ya “mgeni” ambaye thamani yake haitakiwi kuwa tofauti na ya kaka na dada zetu wa karibu. “Mgeni” hapa anawakilisha wale waliotengwa na wasiojiweza. Wote wana haki sawa ya kusaidiwa. Katika “usawa” hakuna habari inasema kuwa wageni wahudimiwe kwanza kabla ya wahitaji wengine, bali neno hili linatutaka kuwasaidia wahitaji wote kwa usawa bila kujali kama ni wageni au la.

Katika Agano la Kale tunasoma kuwa amuoneaye “maskini” humsuta Muumba wake (Methali 14:31) maana wote tumeumbwa kwa mfano wake (Mwanzo 1:26); bali yeye awahurumiaye wahitaji humheshimu muumba wake. Kwa neno hili, Yesu, mhukumu mkuu analitumia kueleza thamani tunayotakiwa kuwapa ndugu. Kwa neno hili kila mtu aliye maskini na mhitaji anavutwa kwa Jesu, maana naye pia ni mfano wake.

Ujumbe wa kuumbwa kwa mfano Yesu, ni wa kushangaza. Maana “wale wenye haki” wanauliza: Ni lini ulikuwa mgeni nasisi hatukukukaribisha?

Neno hili linatukumbusha kuwapokea wageni na kuwakaribisha maana Yesu mwenyewe anaweza kuwa ndani miongoni mwao.

Ukristo na ugeni – wasafiri - taifa la Mungu

Katika vitabu vya Agano Jipya inasisitizwa kuwa, kuwa mgeni na kutokuwa na “nyumbani” ni sehemu ya maisha ya wale waaminio. Mekanisa yanajitambua kupitia simulizi za uhamiaji na zile za kuwa ugenini ambazo ziko kwenye Biblia ya Kiebrania. Mfano ni katika Barua ya Petro ya kwanza, waumini wanapotajwa kama “wageni”. Hali ya kuwa “mgeni” ya Wakristo na kutambuliwa kwao ni sehemu mbili za shilingi moja (1. Petro 1:1,17;2:11).

Haya ndio tunayoyasoma katika barua kwa Waebrania. Barua inaelezea historia za uhamiaji wa Waisraeli kuanzia pale safari ilipoanza, safari ambayo hata sasa haijaisha. Waisraeli waliokuwa na matumaini ya kuishi kwa amani baada ya kufika nchi ya ahadi (Kumbukumbu la Torati 12:9; Zaburi 95:11) – jambo ambalo hadi sasa bado wanalitumainia –, walimsifu Mungu baada ya kukombolewa Misri (na hata sasa). Ndivyo ilivyo kwa wote wanaomsifu na kumwamini Mungu maana wote wapo njiani kutekeleza raha ya sabato (Waebrannia 4:9). Kama Abrahamu, aliyeondoka kwa ahadi ya “kupata pale atakapopata urithi” (Waebrania 11:8–10), ndivyo hata Wakristo wasivyokuwa na “mji udumuo bali twaitafuta ule ujao” (Waebrania 13:14). Kwa hiyo Wakristo tuwe na ari, tutafute tuweze kutazama kutoka mbali tukiyangojea yajayo. (Waebrania 4:11na 11:14).

Ushirika na Mungu na kuwa safari mara kwa mara kunawafanya wamuaminio wahamiaji. Matumaini, matendo na mitazamo yao na tabia zao hazieleweki kwa nyakati za sasa. Kama Paulo anavyoandika, wao ni “wakazi wa mbinguni” (Wafilipi 1:27, 3:20) kwa hiyo wao “ni wageni ulimwenguni”. Wahamiaji wa kidini wanalitazama Kanisa na imani yao, kwa njia hiyo wanaona uhalisia wa uhamiaji na hatima zao. Ni kama wanatazama kwenye kioo ambacho kinawaonesha hali zao wenyewe mbele ya Mungu.

Sisi tunaulizwa: Katika mambo yapi bado tunajisikia wageni na katika yapi tunajiona kufika? Je, tunatakiwa kuelekea wapi na ni mambo gani bado tunayatafuta?



Taifa lisafirio gizani

Tarehe 3. Oktoba, 2013 boti iliyokuwa imebeba watu zaidi ya 500 kutoka Eritrea na Somalia ilipinduka karibu na kisiwa cha Lampedusa. Kisiwani watu walisikia mayowe, lakini watu walifikiri ni sauti za wanyama kutoka baharini. Boti ilichukua dakika chache kuzama na wale walionusurika kufa walikuwa baharini kwa zaidi ya masaa matano wakisubiri kuokolewa. Watu 368 walikufa maji, kati yao 108 walikuwa wamefungiwa ndani ya hiyo boti, akiwemo binti wa miaka 20 kutoka Eritrea aliyekuwa amejifungua muda mfupi kabla ya boti kupinduka. Baadhi yao walizikwa kwenye kisiwa hicho, baadhi ya vitu (nguo, chupa za maji, Biblia, Kuruani, picha za ndugu zao) walivyokuwa navyo wakati wanazama vimewekwa kwenye chumba maalumu cha kumbukumbu.



Taifa lisafirio gizani litaona mwanga, na wale waishio katika giza wataiona nuru.

Isaya 9:1

Ahadi hii ambayo ipo kwenye ujumbe wa salamu za majilio tunaifahamu hata sisi lakini tunaitekeleza vipi kiuhalisia hasa tukiwakumbuka wale waishio gizani kweli? Tafsiri ya Martin Bubers hueleza hili vizuri zaidi “Watu wale waliokwenda katika giza wameona nuru kuu; wale waliokaa katika nchi ya uvuli wa mauti, nuru imewaangaza”.

Je, hili linapokelewa vipi na wale ambao usiku huamshwa na sauti za wanajeshi, wale wanaotafuta chakula kwa ajili ya watoto wao au wale waliopotea jangwani?

Watu wengi wanalazimika kukimbia kwa sababu ya hofu, tumaini lao kubwa ni imani yao. Hivyo si ajabu wale walioangamia Lampedusa walikuwa wamebeba Bibilia na Kuruani. Imani yao ndiyo tumaini lao pekee na wakati huo huo ndio msukumo wao. Tumaini hilo ndilo linalowapa nguvu ya kutumaini maisha mapya yasiyokuwa na hofu, na ndiyo chanzo cha ujasiri wa kuondoka na kuacha yale yote waliyozoea na kuanza upya. Hayo ni maamuzi magumu, lazima tuhoji, binadamu anayefanya maamuzi hayo anakua na lengo gani. Imani yao ni ya kiasi gani kiasi kwamba hawana mashaka kuwa baada ya kuanza safari kutoka “nchi ya mauti” Mungu atawaongoza? (Kitabu cha Nyimbo 361,1)

Wanakuja kwetu na imani kubwa, hivyo ni ushahidi wa imani inayoweza kuhamisha milima na nguvu ya Roho Mtakatifu ambayo hushinda vikwazo vyote. Wahamiaji hao wanasimulia juu ya ile nuru kubwa ambayo hulishinda giza.

Wao wameiona nuru hiyo na wanatuambia: *Kutakuwa nuru!*

1.4 Kanisa la Yesu katika Misioni ya Mungu

Upendo wa Mungu kwa ulimwengu umewekwa wazi kupitia Yesu Kristo. Kupitia kwake na maisha yake ufalme wa Mungu umefunguliwa. Kufufuka kwake kumevunja nguvu za mauti na kuleta tumaini jipya maishani.

Upendo wake Kristo huwavuta watu kwake na kumkaribisha katika mioyo yao. Kristo anawawezesha watu wote, kuishi na kutenda kama ndugu na marafiki wake kwa lengo la kutimiza malengo ya Mungu juu ya uumbaji wake. Theolojia inasema: Yule aaminie ana sehemu yake katika “utawala wa kifalme” wa Kristo. Mfalme huyo ni ndugu na rafiki. Anataka marafiki zake washiriki katika utawala wake kwa kutenda wema ili kuimarisha amani. Matendo ya wema ndiyo yanaufanya ufalme huo uwe imara na wa kuvutia. Moja ya misingi ya ufalme huo ni “kumpenda jirani yako”, kwa kutoa msaada wakati wa shida na wakati wa mateso ya kimwili na kiroho. Lakini pia hata kuthaminiana na kuheshimiana, kuchukua jitihada za kuwaelewa na kuwakubali wengine walivyo pamoja na kujifunza kutoka kwa wengine. Kwa namna hiyo Ufalme wa Mungu unawezesha watu kuishi kwa pamoja bila purukushani.

Lakini maisha ya Yesu si maisha tu yanayokubali maisha ya kila mtu anayekaribia mezani kwake na kuomba kuokolewa; hapana. Yesu kama mtume anasema wazi penye ubaya badala ya wema, uovu, uongo badala ya ukweli na anawataka watu kuitafuta kweli na haki. Kusulubiwa kwake kunatuonesha jinsi sisi wanadamu tusivyoweza bila kutumainia nguvu za Mungu. Utawala wa Roma unamgeuka na matendo yake ya kimungu. Dini tawala inamgeuka Yesu na mafundisho yake. Sheria za kidunia na zile za kidini zinatumiwa vibaya. Maadili ya umma wanashangilia “Hosiana” na wengine wanapiga kelele na kusema “asulubiwe”. Katika hali hii ya kelele na ambapo watawala wanapimana nguvu ni vigumu kutulia na kutoa ujumbe wa kimitume. Ila Yesu ambaye anataka tuingie katika Ufalme wa Mungu ujao anaamini kuwa tutaitafuta njia ya haki na kweli. Anatuamini kuwa tutawashuhudia wengine jinsi njia hii inavyoaminika, inavyoweka watu huru na kuleta furaha.

Kristo pia anatupa nafasi ya kuwa “mashuhuda” kwa kufuata mfano wa maisha yake mwenyewe. Martin Luther alisema “yule aliyebatizwa basi hawezi kukaa bure, maana tayari kasimikwa kuwa mhubiri, mchungaji na askofu na papa...”. Kupitia roho mtakatifu binadamu wanawezeshwa kutoa ushuhuda wa Mungu kwa maneno na matendo ili kuwavuta na wengine kwa Mungu. Lakini pia wanapewa uwezo wa kumuamini Mungu, ambaye awezaye kuondoa mateso na shida na kuleta yaliyo mema na mapya. Kwahiyo inabidi kubadili matendo na mienendo yote iletayo chuki na roho ya uovu. Ni jambo la kufaraji kuona kuwa kurudi kwa Yesu na ufalme wake hauko mbali. Lakini pia tunakumbushwa kuwa “nguvu nzuri” ziko kati yetu hasa kupitia matendo yetu sisi wenyewe.



Dhana ya kitheolojia ya Missio Dei (Misioni ya Mungu) hushinda hali zote, Mission Dei ndio kiini cha imani au kumuamini Mungu, Mungu wa Biblia na Korani kwake ambaye tunamuamini na maisha yetu ya baadaye. Yale waliyoyapitia na kuyoana akina Abrahamu, Musa, Yesu na manabii wote katika Koran na katika Biblia yanatutia moyo leo.

Müzeyyen Dreessen, Afisa Jamii, Muislamu ambaye anajihusisha katika mazungumzo ya mashirikiano ya kitamaduni na kidini kwa miaka mingi

Maana hata Mungu ana mpango na dunia, na hiyo ndiyo maana kanisa lina wajibu wa kuutekeleza huo mpango wa Mungu wa kuibadilisha na kuihudumia dunia. Wajibu huo ndio tunaouita Missio Dei katika Okumene. Kupitia Kristo, Mungu anatushirikisha katika dhamira yake. Jinsi tunavyoishi pamoja kama kanisa, namna tunavyosherehekea, tunavyoshuhudia na kueneza imani na kuyakabili majukumu yetu ndiyo ushuhuda unaodhihirisha ushiriki wetu katika Mission Dei. Sura ya tatu ya toleo hili inaonesha ni hatua gani Kanisa na Sharika huweza kutekeleza.

2. Muelekeo wa maadili ya kijamii

2.1 Mchezo wa nchi wa mioyo

Daniel anapowazia “nyumbani” kwake ni wapi huwazia nchi mbili, Ujerumani na Korea. Daniel ni mjerumani mwenye asili ya kikorea na ni mchungaji wa kanisa la kilutheri katika jimbo la Schwelm. Alizaliwa mwaka 1984 mjini Casrop-Rauxel na kukulia Dortmund.

Daniel amekuwa akijiuliza kwa kipindi kirefu, “nyumbani” kwake ni wapi. Wazazi wake ni wakazi wa Dortmund wa miaka mingi. Wametoshaka na maisha yao na wamekuwa sehemu ya jamii ya hapo Dortmund. Mama yake ndiye alitangulia kuja Ujerumani, mwaka 1967, alikuja kufanya kazi ya unesi na baba yake akaja miaka ya 70 kufanya kazi katika machimbo

Daniel Cham Jung pamoja na mke wake, ambaye naye wazazi wake ni wakorea, wanajiona kama watu wanaoiwakilisha Ujerumani. Ni nchi ambayo kadri muda unavyosogea inakuwa nchi ya makabila, watu wenye asili na tamaduni tofauti. Daniel husikitika pale anapoambiwa kuwa yeye si mjerumani au kuwa Ujerumani si nyumbani kwake. Kwa sababu ya asili yake ya kiasia ni rahisi kumtofautisha na wajerumani wengine. Yeye mwenyewe anasema “Kwa sasa mimi ni wa kipekee” maana watu wanaozungumza naye kwa mara ya kwanza kupitia simu hawawezi kutambua kama ana asili ya uhamiaji. Muonekano wake hawezi kuuficha na mara nyingi hupokelewa kwa mshangao akikutana na watu kwa mara ya kwanza. Mara nyingi pia anatakiwa kujieleza kwa watu juu ya asili yake. Wapo wanaouliza maswali kwa ukarimu lakini hata maswali yao hufikia hatua ya kukera. Kuwa “mgeni” si jambo la kawaida Ujerumani.

Jung anajiainisha kama Mkorea vilevile kama Mjerumani. Wakati akiwa Korea katika mwaka wake wa Ushemasi, aligundua kuwa hata Korea ni nyumbani kwake. Licha ya kuwa kikorea chake si kizuri hakujisikia kama mgeni. Muda huo pia ulikuwa mara yake ya kwanza kuishi kwenye nchi ambayo wakazi wote wana muonekano kama wa kwake.

Tofauti na Korea au hata Marekani, Ujerumani uwezo wa kuitumia lugha ya kijerumani hupewa muhimu sana. Ujerumani watu hujikuta wapo kwenye makundi tofauti kijamii, kulingana na uwezo wao wa lugha za kijerumani. Kwa sababu hiyo wapo wageni ambao hawawezi kushiriki vyema kwenye huduma zinazotolewa kwa sababu ya uwezo wao usioridhisha katika lugha.

Marekani kuna utofauti, huko mtu hapimiwi kwa uwezo wake wa lugha, muhimu ni mtu aweze kujieleza, jinsi atakavyofanya hivyo si muhimu. Wakati mwingine Jung anahisi kuongea kijerumani kwa ufasaha, ni muhimu kuliko mambo mengine yote hapa Ujerumani. Hali hii inapelekea watu kutojiamiani kuzungumza kijerumani. Hata mtu, kuwa na muonekano tofauti Ujerumani bado ni changamoto. Daniel anatomia nafasi hiyo kama nafasi ya kuanza mazungumzo na watu. Daniel ana ndoto “Siku ambayo mkorea wa kwanza ataanza kuichezea timu ya taifa ya Ujerumani kila goli litakalofungwa litakuwa goli la ushindi”.



Katika mpira wa miguu tayari tunaona uwepo wa watu wenye asili, rangi na hata tamaduni tofauti. Hali hii sio ngeni, tena mpaka hata kwenye kombe la dunia. Tukumbuke kuwa wakati wa Kombe la Dunia mwaka 2018 kulikuwa na mjadala juu ya aliyekuwa mchezaji wa timu ya taifa ya Ujerumani Mesut Özil. Mjadala huo ulionesha jinsi mawasiliano yanayohusisha watu wenye tamaduni tofauti yasivyokuwa mepesi kwenye jamii yetu.

Uhamiaji ni jambo la kudumu katika historia ya wanadamu. Uhamiaji pia ni jambo linalotokea dunia kote. Karibia katika nchi zote duniani wapo watu wanaohama. Ila ni wazi kuwa nyakati hizi uhamiaji wa kimataifa uko juu sana. Na katika takwimu za kimataifa watu wanahesabika kuwa wahamiaji pale wanapohamia nchi nyingine na kukaa huko kwa kipindi kisichopungua miezi 12.

Mwaka 2000 takwimu hizi zilionesha kuwa takribani watu Milion 173 walikuwa wahamiaji. Pia ndani ya mwaka huo huo wahamiaji waliongezeka kufikia watu milioni 222, mwaka 2010 walifikia milioni 278. Wahamiaji wengi hawaondoki nchi kwao kwa hiari bali kwa kulazimika. Mwaka 2015 watu milioni 63.5 dunia kote walikuwa wakimbizi, idadi hii ilikuwa haijawahi kufikiwa. Wengi wa wahamiaji hao hupata hifadhi katika nchi jirani. Wanakimbia vita, njaa na umaskini. Takwimu zinaonesha kuwa asilimia 90 ya wahamiaji hupata hifadhi katika nchi zinazoendelea.

Tofauti kati ya wakimbizi na wahamiaji mara nyingi haiko wazi. Wakimbizi ni kundi maalumu la wahamiaji linalohitaji mapokezi maalumu. Wengi wao hukimbilia nchi jirani. Kwa sasa wakimbizi wengi wapo Lebanon, Jordan na Kenya. Miundombinu ya nchi hizo imekwama na kudhoofika kutokana na idadi kubwa hiyo ya wakimbizi.

Zipo sababu pia nyingine ambazo zinawafanya watu waanze kujiuliza nibaki nyumbani au niondoke, mfano ni kutokuwepo na usawa kwenye jamii, utofauti mkubwa kati ya maskini na matajiri, siasa au changamoto za hali ya hewa n.k. Maendeleo katika sekta za mawasiliano na usafiri yanawasaidia watu kufikia maamuzi ya kuhama.

Kuhama na matukio yanayosababisha watu wahame ni mambo ambayo yamekuwa yakitokea nyakati zote. Mfano wa sera za uhamiaji wa kale ni mapokezi ya “*reformed refugees*” Lower Rhein Region wakati wa karne ya 16. Mfano mwingine ni Huguenot waliopokelewa kama wakimbizi wa kidini Ujerumani (hasa sehemu za Berlin na Saarland) wakati wa mapinduzi ya kifaransa.

2.2 Ujerumani: Jamii yenye kujiainisha kuwa ya Uhamiaji

Kutokana na Vita, migogoro ya kidini, njaa, uhasama wa kisiasa na ukosefu wa matumaini ya maisha bora, wajerumani wengi nao walilazimika kuyakimbia makazi yao. Uundaji wa makoloni ya ulaya katika miaka ya 1700 ndio uligubikwa na uhamiaji, hadi watu walivuka bahari ya Atlantiki. Pia kutokana na Umoja wa Preussen mwaka 1817 walutheri wenye imani kali walilazimika kuhamia nchi nyingine kama wakimbizi kwa sababu ya dini yao. Kati ya mwaka 1816 hadi 1914 watu karibu na milion sita walihama kutoka Ujerumani kwenda Marekani, Kanada, Brazil na Australia kwa matumaini kuwa huko wangeweza kujenga maisha bora kwa ajili yao na watoto wao.

Kufuatia mapinduzi ya viwanda mwisho wa karne ya 19, Ujerumani iligeuka kuwa nchi ya kupokea wahamiaji. Nguvu kazi ilitokana na wahamiaji kutoka ulaya ya kusini na kutoka katika vijiji vya Prussia ya Magharibi hasa Poland na Masuria. Watu hao walihamia Ujerumani, kwa sababu wakati huo ilikuwa nchi inayoongoza kiuchumi, hasa katika eneo la Ruhr. Inakadiriwa kuwa mnamo mwaka 1914, kulikuwa na wafanyakazi na vibarua wageni million 1.2 kwenye Dola la Ujerumani.

Mauaji ya kimbari dhidi ya wayahudi hapa Ujerumani (inasemekana wayahudi 34,000 ndio walinusurika mauaji hayo), ni onyo tosha linalotukumbusha kuwa jamii inatakiwa kuwa wazi na kuheshimu utu.

Maajabu ya kiuchumi (ambako eneo la Ruhr, Ujerumani lilishuhudia maendeeo ya ghafla kiuchumi) nayo kwa kiasi chake yalibadilisha jamii ya kijerumani. Kutokana na nafasi za kazi kuwa nyingi, watu wengi kutoka sehemu za magharbi mwa Ujerumani walihamia kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Ujerumani na kuja Rhine Kaskazini–Westfalia. Asilimia 17 ya wakazi wa Rhine Kaskazini–Westfalia walikuwa ni wahamiaji. Utaratibu maalumu wa kuja kwa vibarua (hasa kutoka Ulaya Kusini, Uturuki na Afrika Kaskazini) uliwekwa mwaka 1955 kwa sababu kulikuwa na uhitaji wa vibarua katika machimbo, viwanda vya Schwerin vilivyokuwa na uzalishaji mkubwa. Kwa hiyo kulikuwa na aina mbalimbali za uhamiaji. Rhine Kaskazini–Westfalia ilikuwa katika mabadiliko makubwa.



Hatimaye mitaa yetu ya maduka imechamgaka tena. Kuna maduka mengi madogo na migahawa na hatimaye hatuna tena yale majumba ya michezo ya kijinga. Mimi ninapenda kwenda kuhemea katika duka la Kisiria. Wahudumu ni wakarimu sana.

Mwanamke wa miaka 48

Licha ya sera za uhamiaji zilizokuwa sio rafiki, wahamiaji wengi walibaki. Tena waliitwa “wafanyakazi/vibarua wa kigeni” ikiwa ni njia moja wapo ya kuonesha kuwa uwepo wao si wa kudumu, hali ambayo ilisababisha wasiwe na mshikamano na jamii moja kwa moja. Misaada waliyopewa ilitoka katika makanisa, makundi binafsi ya kutoa misaada na waajiri wao. Hapakuwepo na sera maalumu ya serikali iliyokuwa ikilenga kuwashikamanisha wahamiaji na jamii.

Hali hiyo ilikuwa tofauti kwa wahamiaji walikokuwa na asili ya Ujerumani. Mwaka 1953 sheria maalumu ilipitishwa ajili ya kudhibiti wahamiaji kutoka Urusi waliokuwa na asili ya kijerumani ambao walikuwa wana haki ya kupata uraia wa ujerumani. Tangu miaka ya 60 watu ambao wazazi wao, walikuwa wamehama kutoka Ujerumani na kwenda nchi nyingine, waliruhusiwa kurudi katika shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani. Katika miaka ya 80 hasa baada ya kuvunjika kwa Umoja wa Kisovieti idadi ya wahamiaji iliongezeka. Kati ya mwaka 1992 na 2015 Ujerumani ilipokea wahamiaji milion 1.8 kutoka katika nchi zilizokuwa zikiunda Umoja wa Kisovieti. Kwa kuwa zaidi ya asilimia 50 ya wahamiaji kutoka Umoja wa Kisovieti walikuwa ni walutheri, kanisa letu nalo lilipokea wahamiaji. Kanisa la Kiinjili la Westfalia lilipokea washarika kama 280,000, sawa na asilimia 10 ya washarika.

Kwenye miaka ya 80 ambapo idadi ya wahitaji hifadhi (asylum seekers) iliongezeka kutokana na hali ya kisiasa katika nchi za Balkani, kulifikwa makubaliano ya kisiasa na matokeo yake ilikuwa ni „Asylkompromiss“. Kwa sheria hizo watu walikuwa wanaweza kurudishwa kwao kama nchi waliyotokea ilikuwa iko kwenye orodha ya nchi ambazo zilitambuliwa kama “nchi nje ya umoja wa Ulaya iliyo salama”. Watu ambao waliruhusiwa kubaki, walipewa hadhi ya “anayevulimiwa”. Watu hao bado walikuwa hawashirikishwi katika jitihada za mshikamano na hawakupewa fursa katika soko la ajira. Ni wakati huo ambao mtazamo wa “hifadhi ya kanisa” ulianza kutumika kwa lengo la kutatua matatizo ya haki za binadamu ambayo yalikuwa hayajapatiwa ufumbuzi wa kisheria.

Ili kuendana na vigezo vya sera za Umoja wa Ulaya, mwaka 2005 Sheria mpya ya Uhamiaji ya Ujerumani ilipitishwa. Kwa sheria hiyo raia wa nchi ya Umoja wa Ulaya walipatiwa haki ya kufanya kazi katika nchi zote za umoja huo. Kama ilivyokuwa huko nyuma, wahamiaji wengi waliofika Rhein Kaskazini–Westfalia walitokea Poland. Kwa wakati huu, idadi ya watu kutoka Romania na Bulgaria imeongezeka. Kumekuwa na migogoro kwa sababu ya hali (na haki) yao kijamii kuwa ya shida. Tangu 2007/2008 wakati wa mtikisiko wa kimataifa wa uchumi idadi ya wahamiaji kutoka Italia, Hispania na Ugiriki imeongezeka tena. Tofauti na hapo awali sasa wahamiaji wengi wanawahi kupata kazi.

Pia tumepokea wahamiaji wengi kutoka Syria, sababu kuu ikiwa ni vita inayoendelea katika nchi hiyo. Hata idadi ya watafuta hifadhi na wakimbizi katika eneo la Rhein ya Kaskazini–Westfalia imeongezeka. Kati ya mwaka 2015 na 2016 idadi hiyo ilifika 300,000. Tangu 2017 idadi ya wakimbizi imeanza kupungua tena.



Walikuja kama wakimbizi sasa wamepata mahali pa kuishi

Mimi, ninaishi karibu na chuo kikuu. Hapa wanaishi watu kutoka nchi mbalimbali na wenye rangi tofauti za ngozi. Ninapokuwa kwenye usafiri wa umma najisikia niko kwenye jiji kubwa kwa kuwa wanapanda watu wenye muonekano tofauti tofauti. Miongooni mwao wapo ambao ni kizazi cha pili au cha tatu cha wahamiaji na wakimbizi. Usharika wangu umetoa mara nyingi “hifadhi ya kikanisa”. Usharika unatoa hudumu mbalimbali kama kuwapatia watu ushauri na hata kuwapatia mahali pa kuishi. Huduma hutolewa kwa kushirikiana na usharika wa kikatoliki. Ninapokwenda kufanya manunuzi, nafurahia sana kuona watu wa aina tofauti, wanaovaa hijabu na vibalagashia, wenye kuvaa suruali pana na nguo ndefu. Wao wanazungumza lugha nyingi, ila wanaponiongelesha mimi basi hufanya hivyo kwa kijerumani.

Mitaa hatari

Kila wiki ninakwenda kwenda upande wa pili wa mji na huko ninakutana na wahamiaji. Kuna mitaa ambayo wahamiaji wengi walipewa makazi, mitaa hiyo imegeuka kuwa kuwa makazi hatarishi. Watu kutoka nchi zaidi ya 60, huishi huko. Kwenye mitaa hiyo kuna migogoro na maisha sio mazuri. Mara nyingi nikipanda basi au treni kunakuwa na kelele, watu wanaongea kwa sauti za juu wakiwa wanaongea na simu. Wakati mwingine nasikia vijana wanavyosimuliana kwa kujiamini jinsi wanavyowakimbia na kuwakwepa polisi. Mazungumzo yao yanafanyika kwa lugha za mtaani. Wakati mwingine mazungumzo yao ni ya kutisha, mfano kijana fulani alimpigia “mshikaji wake” aje wakutane mahali kwenda “kummaliza” mtu mwingine. Wakati mwingine vijana hao huoneshana visu vyao, kwa majigambo. Kusema ukweli usiku nikiwa safarini na kulazimika kupita katika mitaa hiyo huwa sina amani kabisa.

Mwanamke wa myaka 75.

Mjadala juu ya changamoto za uhamiaji kwa kiasi fulani umechukua mwelekeo ambao unalenga kusambaza chuki dhidi ya wageni na ambao una nia za kiubaguzi. Changamoto hizo pia zimeibua maswali juu ya utaiifa.

Changamoto hizo zimetufikisha mahali ambapo hata misingi ya haki za binadamu inaanza kutiliwa mashaka. Hasa nguzo kuu ya haki za binadamu ambayo husema wazi kuwa thamani ya watu wote ni sawa bila kujali mtu atokapo wala kabila lake.

Kwenye jamii yetu lipo kundi la watu wanao waona wahamiaji kama tishio. Kundi hili linaonesha tofauti baina ya wahamiaji na “sisi”. Hilo ni tishio na jambo la kutia wasiwasi.



Nikiwa napita katika mtaa wenye maduka mjini, sioni hata duka moja la kijerumani. Naona maduka ya kigeni tu, migahawa ya ajabu ajabu, harufu nisizozijua na ninasikia lugha nisizoielewa. Siwaoni hata wajerumani mitaa hiyo. Tunaishi wapi kwani?

Mzee wa miaka 70

Mara nyingi watu wanaokuwa na mtazamo huo ni wale ambao tayari wametengwa na jamii au ni watu ambao wana misimamo ya kihafidhina. Watu hawa hupenda kushiriki katika majadiliano na michakato ya kisiasa. Shida kubwa ni watu ambao wanasisitiza nchi kuwa ya wajerumani tu.

Mfano kwenye chama cha AfD wapo wanachama wa makundi tofauti. Lakini kundi la wale wanaotaka “ujerumani ya wajerumani” ndilo lenye nguvu katika chama.

Tofauti hizi zinaonyesha wazi kwamba kuna umuhimu wa kuchukua hatua mbalimbali dhidi ya makundi ya mrengo mkali wa kulia.

2.3 Jukumu la Dini la kuimarisha utofauti ndani ya jamii yetu



Ujenzi wa msikiti kama ishara ya kujisikia nyumbani” makazi mapya

Tangu mwaka 1982 chama cha waislamu Dortmund-Hörde kilianzisha mchakato wa kujenga msikiti. Mwaka 2003 chama cha waislamu kilianza mawasiliano na mamlaka ya mji kwa ajili ya kutumia eneo ambalo lipo karibu na Grimmsiepen. Eneo hilo lilikuwa wazi na lilikidhi matumizi.

Lakini umma ulivyopata habari ya mpango wa kujenga msikiti eneo hilo, ulizuka upinzani. Kilele chake ilikuwa ni Septemba 11,2001. Sahihi za watu waliopinga zilikusanywa ili kuzuia ujenzi huo. Kanisa la kilutheri liliitisha mkutano na watu waserikali, majimbo ya kanisa na vyama vya kiislamu. Hata ofisi ya mji ilikaribisha watu kwenye vikao na mijadala, ili watu waweze kupewa taarifa kamili juu ya mpango wa ujenzi wa msikiti huo. Watu zaidi ya 250 walihudhuria vikao hivyo.

Waislamu waliuima sana, maana walijiskia kuogopwa na kutuhumiwa mabaya. Hawakuelewa ni nini kilichokuwa kinawafanya wajerumani wapinge ujenzi wa msikiti na kuwatilia mashaka. Waislamu wao walikuwa wanajiona kama sehemu ya jamii, yaani hawakujiona kama wageni tena.

Wakazi wa Hörde, walitoa msimamo wao wa pamoja kufuatia maandamano yaliyofanyika nchini kote kupinga ujenzi wa msikiti huo. Maandamano hayo yaliitishwa na neo-nazis. Wakazi wa Hörde walipinga vikali misimamo ya neo-nazi, kwa kuitisha maandamano kwa kushirikiana na chama cha waislamu. Watu zaidi ya 1,000 walishiriki katika maandamano hayo. Watu waliandamano wakiwa wameshikana mikono. Wakati wa maandamano hayo waislamu walikuwa wamebeba mabango yenye maandishi mbalimbali, mfano “Nyumbani kwangu ni Hörde, sina mahali pengine” na “Mimi sio mgeni.

Wakati maandamano yakiendelea, uliibuka mijadala juu ya mpango na utaratibu wa ujenzi wa msikiti huo. Hatimaye mipango ya ujenzi ilipitishwa baada ya vyama vya SPD na CDU kuhimiza na kukumbusha juu ya uhuru wa dini na kuabudu.

Tangu ujenzi wa msikiti kukamilika, maandamano yamepungua, kinachongezeka ni ugeni kutoka miji jirani. Wageni wengi wanakuja kuuona msikiti huo ambao umekuwa ni alama ya eneo la Hörde. Kwa jinsi ulivyojengwa kwa kuvutia, una madirisha makubwa na marefu kiasi kwamba watu walioko nje wanaweza kuona yanayojiri kwenye msikiti. Kinachowavutia watu hasa ni kwamba msikiti huo umejengwa kwa michango binafsi.

Kitu ambacho bado kinakosekana ni minaret. Kwa tahadhari, mji umesaini mkataba na uongozi wa msikiti huo. Katika mkataba huo wamekubaliana kipimo cha sauti (decibel) na kuwa wito kwa sala unaruhiswa kusikika mara moja kwa wiki, siku ya Ijumaa.

Licha ya kuwa uhamiaji unakuza utofauti wa watu katika jamii pia una changamoto zake. Tukumbuke kuwa wageni huja na mila na desturi, dini zao ambazo ni tofauti na zetu.

Utofauti huu ni changamoto hata kwa wahamiaji wenyewe maana na wao hujikuta hata dini zao, maadili na desturi zao ni tofauti na zile za eneo wanapohamia. Tena ni lazima watii taratibu za nchi na kufuata misingi inayoelezwa hata kwenye Katiba ya nchi, ikiwemo usawa na haki za kufanya maamuzi.

Dini na Jumuiya za kidini zinatakiwa kujiuliza maana ya kuishi kwa pamoja, kama majirani wenye utofauti lakini wenye wajibu wa kuhakikisha kuishi kwa pamoja kwa amani. Kwa hiyo kanisa, linatakiwa kuchukua jukumu la kuwezesha watu kutambua tofauti zilizopo na kubainisha misingi ya kimaadili inayowakutanisha wazawa na wahamiaji.

Ujerumani, nchi isiyo na dini inatafuta kanuni na njia ambazo zinawezesha kustawi kwa dini mbalimbali nchini. Wapo watu wanaotoa hoja kuwa dini (au imani) sio suala linalotakiwa kupewa nafasi katika majadiliano ya umma ili kulinda “neutrality” ya nchi. Kupitia dini, upo wajibu wa kuhakikisha maisha ya amani kati ya watu wenye dini tofauti inadumishwa.

Lakini hata madhehebu ya dini za kikristo yanaongezeka. Hili ni jambo geni kwetu. Tangu wakati wa vita baina ya madhehebu wakati wa Matengenezo ya Kanisa Ujerumani ilikuwa na madhehebu machache. Katika jimbo la Rhein Kaskazini-Westfalia, madhehebu yaliongezeka baada ya wafanyakazi wa kigeni kufika wakati wa mapinduzi ya viwanda na wahamiaji na wakimbizi kufika wakati wa vita ya pili ya dunia.

Wakati wa sasa, tunashuhudia ukaribu, urafiki na ushirikiano wa makanisa makubwa na makanisa madogo na hata makanisa ya madhebu mengine. Wakati huu wahamiaji wanaokuja kwetu nao huja na dini, madhehebu na mila na desturi tofauti. Wahamiaji wanapata mazingira yanayowawezesha kuendelea kuabudu imani zao kwenye jamii ambayo nayo ina dhehebu lingine la kikristo au hata dini nyingine. Kwa namna hiyo wahamiaji wanaweza kutunza sehemu ya “nyumbani” kwa kuendelea kuabudu walivyozoea kwa lugha wanayoielewa vizuri.

2.4 Njia za kuwezesha umoja na ushirikiano wa watu wenye asili tofauti

Jamii zenye kupokea wahamiaji lazima zitengeneze mazingira ambayo yanawezesha wahamiaji na wenyeji kuwa na mahusiano mazuri. Hili ni jukumu la muhimu ambalo kwa bahati mbaya hapa Ujerumani lilikuwa halijapewa kipaumbele. Tangu mwaka 2007 Ujerumani imekuwa na mchakato wa umoja na ushirikiano wa watu wa asili tofauti (integration plan) ngazi ya taifa kuanzia mwaka 2008. Tangu mwaka 2008 pia zipo taarifa rasmi juu ya maendeleo (na maendeleo hasi) ya umoja huo.

Neno “umoja” hutumika mara kwa mara bila maana yake kueleweka na bila kujua nani anatakiwa kuchukua jukumu gani katika mchakato huu wa kufanikisha umoja wa watu wenye asili, dini pamoja na mila na desturi tofauti. Umoja ni mchakato unaotakiwa kutoka pande zote mbili husika; wahamiaji na wenyeji. Ili kufanikisha umoja lazima kuwe na fursa sawa (za elimu, haki, afya n.k.) kwa wazawa na wageni. Ni muhimu kutofautisha “umoja” na “usimilishaji”. Umoja na ushirikiano ni mchakato unaowataka wageni na wazawa kushiriki sawa. Ili kufanikisha mazingira rafiki na umoja lazima kuwepo na matukio na nafasi za wageni na wazawa kukutana na kubadilishana mawazo. Mfano katika jumuiya za kidini, klabu za michezo, mazingira ya kazi na ujirani mwema. Umoja na ushirikiano ni mchakato unaotakiwa kuanzia ngazi za chini za jamii.



Mimi nimekuwa nikiwashauri wafanyabiashara wa kituruki kufanya kazi na sisi kwenye kamati zetu ili kufanikisha hali ya kujisikia wamoja. Ila ni lazima kuisitiza kuwa yale yanayojiri na kusemwa msikitini yanaweza kuathiri au kufanikisha umoja. Si jambo la kupinga tena, waislamu ni sehemu ya jamii ya kijerumani. Uislamu hautambui mipaka kati ya kanisa na serikali. Kwetu mipaka hiyo ni muhimu sana na hata katiba yetu inashikilia msingi huo. Kwa hiyo ni sawa kujiuliza kama kweli Uislamu unaendana na misingi yetu ya uhuru na demokrasia. Mimi sioni kama Uislamu unaweza kufikia hatua ya kuwa sehemu ya jamii yetu. Kwa mtazamo wangu, Uislamu ni kizuizi cha umoja.

Friedhelm Müller, Kaimu Mwenyekiti wa chama cha CDU, Umoja wa Wafanyabiashara jimbo la Rhein Kaskazini-Westfalia na mmoja wa waanzilishi wa jukwaa la wajerumani – waturuki



Tukiwa tunajua kuwa tunaweza kusali kwa pamoja msikitini au kanisani, basi twamwamini Mungu mmoja. Kwa hiyo inatubidi tusiombe tu kwa pamoja ila tutoe huduma za kidiakonia kwa pamoja maana hivyo ndivyo waaminio wanavyotakiwa kuishi- kuishi imani yetu

Agim Ibishi, Afisa Ustawi wa Jamii, , mwislamu anayefanya kazi Kituo cha Diakonia cha Jimbo la Kilutheri la Herford

Kuna tofauti kati ya “ushirikiano wa kibinafsi” (individual integration) na “ushirikiano wa kimiundo” (structural integration). Ili kupima uwezo wa mtu kufika kwenye jamii vifuatavyo huangaliwa: elimu hasa uwezo wake wa kutumia lugha ya pale alipohamia, kazi na kipato chake na uwezo wake wa kutumia fursa za kiuchumi. Ushirikiano wa kimiundo ni pale ambapo mgeni hukubali maadili ya jamii aliyohamia pamoja na kukubali na kufuata taratibu zilizowekwa ili kufanikisha kuishi kwa amani. Huu pia ni mchakato wa kisiasa. Haki za binadamu ndio msingi (Kifungu cha 1–20 cha Katiba ya Ujerumani) wa maadili ya jamii ya Kijerumani. Misingi hiyo lazima ifuatwe na kuheshimiwa na wahamiaji wote wanaotaka kuwa “nyumbani” hapa Ujerumani. Misingi hiyo ina historia ndefu ambayo inahusishwa na misingi ya dini ya Kikristo, lakini ambayo mtu wa dini yeyote anaweza kuifuata na kuiheshimu. Pia zipo mila na desturi za jamii yetu ambazo lazima ziheshimiwe. Mfano ni siku kuu na majira ya kalenda za Kikristo ambazo ni sehemu ya utamaduni wetu. Lakini pia yapo maadili ya jamii yetu yaliyotokana na historia ya nchi yetu, hasa maangamizi makuu dhidi ya Wayahudi wa Ulaya. Historia hii inatukumbusha sisi, kama nchi kutokubali wala kushiriki katika aina yoyote ya Anti-Semitismus pamoja na kuitambua nchi ya Israeli.

Wahamiaji wenyewe pia wajitahidi kutunza lugha na tamaduni zao. Jambo hili sio kikwazo cha kufanikisha umoja; tena lugha na tamaduni hizi zinaweza kuwa faida kwa jamii yetu.



*Sifahamu mila na desturi za kiarabu ila Waarabu
ninaokutana nao ni wakarimu sana.*

Mwanamke wa miaka 42

Kwa hiyo ili kufanikisha mahusiano mazuri kati ya wahamiaji na wenyeji lazima pande zote mbili ziwe tayari kuheshimu utofauti wao lakini ni lazima taratibu na maadili ya msingi ya jamii inayokaribisha wageni ziheshimiwe. Utunzaji wa mila na desturi za wageni sio tishio bali ni fursa nzuri kwa jamii yote kwa ujumla.

Wahamiaji hawatakiwi kuchukuliwa kama wapokeaji wa misaada ya kiserikali, bali kwa kupewa fursa sawa na wenyeji wao pia wanapata uwezo wa kujitegemea na kuchangia katika maendeleo ya jamii iliyowakaribisha. Ndio maana mashirika na jumuiya za wahamiaji ni wadau kwenye mchakato wa kutafuta njia za kuwezesha umoja na ushirikiano.

3. Misukumo kwa kanisa na jamii

Msimu wa vuli mwaka 2015, walipoingia wakimbizi karibu 900,000 Ujerumani; makanisa yalionyesha matokeo ambayo ujio huo ulikuwa nao katika maisha ya imani. Wazee wa makanisa, wajumbe wa sinodi na viongozi wa kiroho walitoa wito kwa jamii kuwa wazi na tayari kuwakaribisha wakimbizi. Watu wengi walijitolea kutumia muda na nguvu kuhakikisha wakimbizi wanapokelewa na kukaribishwa vizuri. Sharika zilitoa vyumba kwa ajili ya malazi. Hata mpaka sasa bado kuna kozi za lugha zinaozendeshwa na ufadhili wa aina fulani. Hivi vyote vinasimamiwa na watu wa kujitolea. Vivyo hivyo kuna watu wanaowasadia wakimbizi katika masuala ya kisheria au katika kozi za kuchangamana katika jamii (*integration courses*). Zipo pia ibada zinazofanyika katika lugha mbalimbali. Kujihusisha kwa makanisa kwa ajili ya wakimbizi hakujakosa athari. Ufahamu wa wakristo na matarajio yao kwa kanisa vinabadilisha uhai wa kanisa lenyewe

Kwa kufuata sura ya 1.4, tunaposoma kuhusu msingi muhimu ambao pia ni muongozo wa kanisa, tunataja mifano ya miradi na uzoefu kutoka katika Kanisa la kiinjili la Westfalia, ambayo inachochea mijadala na tafakari.

3.1 Kuwa kanisa pamoja



Usharika wa Lydia unataka kuwa wa kimataifa

„Kuwa kanisa pamoja – kuwa usharika wa kimataifa” – Kauli mbiu hii ndiyo mkakati wa usharika wa Lydia huko Dortmund. Kwa mujibu wa orodha ya washarika, miongoni mwao kuna wakristo wa kiume na wakike kutoka mataifa 62. Tangu mwaka 2016 usharika huo upo katika kuwatambua na kuchangamana na watu wenye asili za uhamiaji katika shughuli zote za usharika huo. Hali hii ambayo tayari ni ya kawaida katika shule za awali na katika ibada za watoto inatakiwa kuwa hivyo pia katika idara nyingine za usharika. Kuanzia mwaka 2020 mkakati huo utadhihirika hata katika muundo wa uongozi wa usharika, walau nafasi mbili katika kamati ya usharika zinatakiwa kugombewa na watu wenye asili za kimataifa. “Tunataka yale yaliyo yetu kuyasuka, kuyaunganisha na mageni” – hivi ndivyo Usharika unavyoeleza malengo ya dhana hiyo.



Usharika uzungumzao Kiajemi huko Paderborn

Takribani wakristo 50 hadi 70 wanaoongea kiajemi huko Paderborn husali ibada zao katika kituo cha Lukas kwa lugha yao na huwa na masomo ya biblia mara moja kwa mwezi. Mara moja kwa mwezi hufanyika ibada za pamoja katika Usharika wa Lukas ya kikundi hiki na washarika wa usharika huu wa kiinjili. Katika ibada hizi, alama zilizo za umoja kama vile Ubatizo hutendeka, miaka (hapa kuna namba imesahaulika au ndivyo ilivyo?) iliyopita watu mia na wamebatizwa. Lakini pia katika ibada watu hushiriki pamoja chakula cha Bwana. Mchungaji Mehrdad Sepehri Fard aliyekuwa akijitolea kipindi cha nyuma amepata kazi ya muda ya kuyasimamia mahusiano haya tangu msimu wa vuli wa 2017: “Huduma ya kiroho kwa wakristo waongea Kiajemi”. Lakini msaada unaweza kuhitajika hata kwa wakristo walioko majimbo mengine. Wakristo waongea lugha nyingine na wenye asili kutoka kwingine hujisikia nyumbani ndani ya kanisa la huku, wanaposikia nyimbo na kuwa na ibada ambazo zinaendana na zile walizozioea kwa kutumia lugha yao. Ndiyo maana sharika nyingi zaidi zinazidi kutumia lugha tofauti tofauti katika ibada. Kwa jinsi hiyo, Wakristo watokao nchi nyingine hujisikia wameguswa.

Sharika zilizojulikana kama “Sharika za lugha nyingine na watu wenye asili nyingine” ambazo zilianza kuwepo tangu miaka ya 1970 zilidumu katika ujirani mwema na sharika za kanisa la kiinjili. Baadhi ya makanisa hayo yalipanga majengo au vyumba vya makanisa na mengine yalikuwa jirani na nyumba za kanisa. Uhusiano huu ulikuwa changamoto ya kilugha na tamaduni, ila pia ya kitheologia. Kwa sasa sharika za wahamiaji zipo katika kizazi cha pili. Watoto na vijana wanazungumza kijerumani kwa ufasaha kuliko lugha mama za wazazi wao. Wamechangamana vizuri katika jamii ya kijerumani. Nia ya kufanya kazi kwa pamoja na makanisa ya wenyeji ni kubwa. Hata sasa, kwa msaada wa kanisa la Rhein Kaskazini-Westfalia, kuna mtandao mzuri wa utendaji kazi za pamoja.



Mkutano wa kimataifa wa makanisa (IKK)

Mkutano wa kimataifa wa makanisa (IKK) ambao unajumuisha reformed churches 160 ambazo hushirikiana na kufanya kazi kiokumene kwa kushirikiana na kanisa la Rhein na lile la Westfalia. Kundi hilo la makanisa linahusisha sharika za kipentekoste, kikirismatiki, kipresbiteri, kimethodisti hata kanisa ya nje ya kilutheri na yale ya kimageuzi. Makanisa yanayokubaliana na msingi wa Halmashauri ya Kiokumene ya Makanisa (kwa kiingereza World Council of Churches) yanaweza kujiunga na IKK: Msingi huo unasema:

“Sisi tunajitambua kama jumuiya ya makanisa yanayomkiri Bwana Yesu Kristo kuwa ni Mungu na Mwokozi kadiri ya Maandiko, na kwa sababu hiyo yanajitahidi kutekeleza kwa pamoja wito unaoyaunganisha yote kwa utukufu wa Mungu pekee: Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.”

Makanisa na sharika ambazo ni wanajumuiya huwapa nafasi watu wanaotoka katika kundi la lugha na utamaduni mmoja kujisikia nyumbani wakiwa ugenini. Makanisa na sharika hizi ni sehemu ambazo wageni wafikao huweza kufikia na kusaidiwa kujiweka sawa katika mazingira mapya wanayokuwa wameingia. Hata kazi za kuwasadia wakimbizi zina nafasi ukubwa kwa makanisa na sharika hizi.

Jumuiya ya IKK pamoja na makanisa ya majimbo ya Rhein na Westfalia hutoa nafasi za kujiendeleza kielimu na pia hutoa ushauri. Wigo wa misaada inayotolewa ni mpana, unahusisha huduma ya kuwabatiza watafuta hifadhi (na wakimbizi) na katika misingi ya Matengenezo au hata uelewa wa Misioni. Mabadilishano ya namna hiyo ni ya msaada mkubwa katika kuelewa tofauti za kitamaduni na kutuunganisha pia.

Kuunganika na sharika nyingine na umoja wa kikristo ulimwenguni ni msingi wa uelewano wa sharika na makanisa. Haya yanaonekana katika mistari ya mwanzo ya nyaraka za Agano Jipya: Neema ya Bwana iwe nanyi, na amani ya Mungu baba yetu, na Yesu Kristo.” Na Paulo anaandika “Usharika wa Mungu Korintho... wale wote waliitao jina la Bwana Yesu Kristo kila mahali, wakiwa kwetu au kwao” (1. Wakorintho 1,2,3) Usharika wa wenyeji ni sehemu ya kitu kimoja kikubwa. Ule umoja na Kristo, hukumbatia na huhusianisha kupita mahusiano mengine ya kawaida, ya kijamii na ya kitaifa. Maneno haya yanasomeka katika vitabu vya Jumuiya ya Makanisa ya Kilutheri ya Ulaya. Kanisa la Kiinjili la Westfalia ni miongoni mwa makanisa anzilishi ya jumuiya hiyo. Hii ndiyo dira ya kanisa ambalo lina uzoefu thabiti na la kiulimwengu ambalo linatambua umoja wake katika Kristo na kwa pamoja ni mwili mmoja wa Kristo. Iwapo mtu atafuata dira hii, ndipo inapokuwa wazi ya kuwa Mungu hutuletea kitu kupitia utofauti wa mtu mwingine. Kupitia mambo mageni, Mungu mwenyewe hutupa changamoto na kutunufaisha. Katika hali ya ugeni Mungu hukutana nasi: Mlinipokea.

Kupitia magumu yote sharika za makanisa yetu, vikundi na mtu mmojammoja hutambua na huyapokea yaliyo mageni na kwa njia hiyo huanza kijihusisha nayo. Kwa namna hiyo watu hupata manufaa ya kibinadamu, ya kimaudhui, ya kitheologia na ya kiroho. Mifano ifuatayo inachochea kutafuta majibu yafaayo katika usharika ama katika mazingira ya kazi.



Mwananchi mwenzetu na jirani wa nyumba moja? (Waefeso 2, 19)

Wakati wa kuandaa sherehe za kukaribisha mwaka mpya, barua pepe inaingia “hivi kuanzia sasa sherehe ya kukaribisha mwaka ni ya kimataifa? Basi kama ni hivyo sisi hatushiriki, hapatakuwepo na kwaya, maana mambo yalivyokwenda ovyo mwaka jana- hapana sisi hatutaki kabisa.”

Kinachofuata ni mikutano ya dharula, vikao kwa njia ya simu na mazungumzo. Matokeo yake hayaridhishi- sababu ilikuwa “sauti” vyombo vya bendi ya waafrika havikuwa vinaendana na vyombo vyetu sisi. Sauti zinajirudia na kugomagoma na hata kuna watu wanaongea kwa sauti ya juu, vyombo vyetu vililemewa – ombi-je, mnaweza kupunguza sauti au kuongea kwa sauti ya chini?

Kwa hivyo nyinyi si wageni wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu.

Jumapili mchana msharika wa usharika wa watamali kasimama mlangoni “Mchungaji wetu hataki tena washirika waendeleo kushiriki katika ibada za pamoja, ibada za mataifa mbalimbali. Anasema kwenye ibada hizo kuna tamaduni chache za kitamali. Pia muda anaopewa mchungaji wetu kwenye hizo ibada hautoshi. “Mchungaji huyo alitakiwa kushiriki katika sherehe za kukaribisha mwaka. Yeye pamoja na viongozi wengine wa kidini walitakiwa kutoa baraka kwa lugha za wanaobarikiwa. Mchungaji huyo hakufika kwenye hiyo ibada.

Wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu?

Wasiwasi na msisimko kwa mchungaji wa usharika wa Kikorea. Makubaliano yalikuwa kwamba yafanyike mahubiri ya aina ya mazungumzo. Yeye pamoja na mchungaji wa usharika wa kitamali waliombwa kuendesha mahubiri hayo. ”Mahubiri ninayafanya peke yangu, sasa nawezaje kuhubiri na mtu mwingine?” Huu ni utata. Tunakubalina kukutana ili kuandaa hayo mahubiri. Makubaliano: mwanafunzi wa kitamali atagusia masuala ya kidunia na mchungaji wa kikorea atazungumzia masuala ya kiroho.

Wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu?

Hatimaye siku ya ibada inafika. Bendi ya kiafrika imeelewa tulichowaomba, wanaimba acappella, zaidi ya gita hawatumii chombo kingine. Vyombo vyetu vinafanya kazi vizuri, shukrani kwa uwepo wa mzee wa kanisa mwenye uzoefu na vyombo vya muziki. Hata mahubiri ya aina ya mazungumzo yanapokelewa vizuri. Hata Mchungaji wa kitamali ambaye alikuwa ametoa taarifa kuwa hatahudhuria anafika katika ibada na anatoa baraka kwa wale waliosimama mbele yake. Hata muwakilishi wa usharika wa kitamali wa Duisburg anashiriki katika ibada.

Wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu!

3.2 Kusherekea imani kwa pamoja



“Ninataka kufikiri mwenyewe” – hivi ndivyo anavyosema Hasan Nabeel, mwimbaji katika kwaya ya Luther-Oratorium.

Mpakistani huyo ni mmoja wa waimbaji wa kipekee katika kwaya hiyo. Hapo awali Hasan Nabeel hakujua Luther ni nani. Kijana huyo mwenye umri wa miaka 31, ambaye anaishi Ujerumani tangu mwaka 2015 anasema “Sasa najifunza zadi juu ya Luther”. Katika kwaya amejifunza na kuijua imani yake mpya, amejifunza lugha na amepata marafiki.

Akiwa Pakistani, Nabeel alikuwa tayari amekutana na dini ya kikristo. Pamoja na rafiki yake walitembelea kanisa hukohuko Pakistani. Familia, ambayo ni ya kiislamu ilimzuia kushiriki katika ibada za kikristo. Ndipo alipoamua kukimbia. Nabeel alibatizwa Agosti 2016. Kijana huyo mnene, aliyekuwa akifanya kazi kama fundi wa kuchomelea vyuma hutabasamu sana wakati akisimulia juu ya hayo. “Nilisubiri kwa muda mrefu. Kabla ya ubatizo wangu, nilikuwa nawaza juu ya yale niliyopoteza kutokana na kukimbia kwangu, ila sasa naona niliyopata.”

Wimbo anao upenda sana wa kwaya hiyo unaitwa “kufikiri mwenyewe”. Maneno ya wimbo huo yanasema “Nataka kufikiri mwenyewe-mimi na Mungu pekee.” Na kinachomvutia kwa Luther ni Ujumbe wake wa kuwa huru: “Tunaweza kufanya maamuzi wenyewe na si lazima tuwe kama watu wengine. Tunao wajibu kwa Mungu tu.”

Ibadani watu wanakusanyika ili kuwa karibu na Mungu, kumsifu, na kuleta shida zao kwa njia ya sala mbele za Mungu. Wanatafuta pumziko, faraja, umoja kati yao na Mungu na mahubiri ambayo yanagusa uhalisia wa maisha yao. Watu wengi wanapata jumuiya, nguvu na hata “nyumbani” kwenye ibada.

Ibada inaendeleza desturi. Sharika nyingi hutambua kuwa Ibada ni msingi wa maisha ya usharika. Ndio maana ni vyema watu wenye desturi tofauti za kusherehekea ibada wakakutana. Ibada ikisherehekewa kama “wajibu na ushiriki wa washarika wote” basi kunaweza kutokea mabadiliko hasa kupitia kusikia sauti na nyimbo mpya, kusikiliza neno la Mungu katika lugha zingine na kupeana ushuhuda.

Sherehe yenyewe ya ibada ni “ngeni”. Sala na liturgia ni desturi zenye asili ya Israeli, Syria, Byzantium, Roma na Afrika Kaskazini zimeongezwa katika ibada zinazofanyika Westfalia. Ibada yetu ya kiiinjili inaonyesha harakati ya kiokumene za milenia 2, hilo huonekana hata kwenye muziki na uimbaji.

Muziki wa kiprotestanti ulienezwa nje ya nchi kupitia misioni na kazi iliyofanyika na kwaya za matarumbeta. Mekanisa ya wazawa yaliupokea muziki wa kiprotestanti na kuufanya sehemu ya desturi zao. Kinyume chake, muziki na nyimbo za kiinjili kutoka nje zimefika kwetu na zimekuwa sehemu ya vitabu vyetu ya nyimbo. Muziki unavuka mipaka ya kitamaduni na lugha. Kwaya ni njia nzuri ya kujenga usharika. Uchaji wa Mungu, mahuburi ya wakristo wenye lugha na asili tofauti na zetu unaweza kuwa wa kushangaza lakini pale sauti na muziki unapoanza, tunaona jinsi kumsifu Mungu kunavyowaunganisha watu.

Muhimu ni msimamo wa usharika: Je, ibada ni “mahali pazuri” ambapo vitu vizuri tu vinapewa nafasi au ni mahali ambapo watoto wote wa Mungu hufika na kutuliza kiu na njaa zao na kuufuraia utukufu wa Mungu?



Vitu vinavyoweza kusaidia katika ibada:

(kama liturugia katika lugha mbalimbali, sala, tafsiri za Biblia, ubatizo wa wakimbizi, masomao ya imani na miongozo ya kusherehekea ibada ya chakula cha Bwana) vinapatikana mtandaoni.

3.3 Kuieneza na kuishuhudia imani



Maryam anasimulia:

Mimi nimezaliwa katika familia ya kiislamu, lakini wakati nikiwa Iran nilikuwa napata shida sana na utofauti wa mwanamke na mwanamume katika dini ya kiislamu. Mfano halisi ni nafasi ya mwanamume na mwanamke mbele ya mahakama. Ndio maana nilimkataa “Mungu asiyenipa haki” na kuamua kuishi bila imani. [...] mahali tulipokuwa tukiishi (baada ya kufika Ujerumani), watoto wangu walikutana na Familia S, na kuanza kuzungumza juu ya dini ya kikristo. [...] Siku moja nami nilisikiliza mazungumzo yao. Walisimulia juu ya habari ya wanaume waliokuwa wakitaka kumpiga mawe mwanamke mzinzi. Yesu alikuja na kuwazuia wanaume hao na akawambia asiyekuwa na dhambi ampige kwa jiwe. [...] Maneno haya ya Yesu yalinigusa. Kuanzia hapo niliwasiliana na ofisi zinazotoa ushauri kwa wakimbizi Iserlohn juu ya jumuiya za kikristo.

Ibada ni sehemu ya watu kukutana ili wawe karibu na Mungu, kumsifu, kumuomba na kuleta shida zao mbele zake

Kwa kufuata maisha ya Paulo, maisha ya mkristo hufata misingi hii: Upendo wa kindugu, tumaini, sala za mara kwa mara, ukarimu na upendo kwa wageni. Matendo hayo ndio shududa ya imani. Lakini uhalisia wa sasa pia unatutaka katika ibada kupinga vikali chuki, na kuhakikisha chuki haitawali maisha yetu. Tumekua tukiona wageni na wale wanaojitolea kuwasadia wakishambuliwa na chuki kupitia mijadala mbalimbali. Sehemu nyingi duniani wakristo wanateswa na kunyanyaswa. Watu wa dini mbalimbali wanateswa wakipigania haki za kuabudu. Kanisa letu linatambua jukumu lake la kuwa upande wa wale ambao utu wao hauthaminiwi kwa sababu ya utofauti wao. Moja ya chanzo cha mtu kubaguliwa ni dini yake. Uhuru wa dini ni haki ambayo lazima ilindwe duniani kote.

Hata kazi ya kanisa ya kuelimisha ni aina ya ushuhuda wa Injili. Kazi ya kanisa ya kutoa elimu ni kazi muhimu na ya kudumu. Kazi hii inalenga kukuza uwezo wa watu wa kufanya maamuzi na matendo ambayo yanaenda na maisha ya kikristo. Zaidi ya yote inalenga kulifahamu neno la Mungu kwa kusoma Biblia ambamo tunakutana na simulizi na picha ambazo zinatusaidia katika maisha yetu sasa. Simulizi na mifano iliyokuwa ikitolewa na Yesu, juu ya ufalme wa Mungu ni simulizi zinazotia moyo na kutupa tumaini. Simulizi hizi zikipata nafasi ndani ya masikio na mioyo ya watu, itakuwa nuru ya Injili. Mahali ambapo watu wageni wanaweza kusimulia historia zao, mahali hapo mambo na uzoefu unajipanga wenyewe. Tena katika mazingira hayo wenyeji nao wanapata nafasi ya kusimulia historia zao na kubadilisha mawazo na uzoefu na wageni. Historia zenye simanzi au ugumu fulani, pia zinaweza kusimuliwa kama mazingira ya siri na faragha yakipatikana.



Kikundi cha wakristo kutoka nchi za kiislamu kinakutana kila mwezi pamoja na washarika wa kanisa la eneo hilo kwa ajili ya Bible-study. Mazungumzo hayaendi haraka na yanataka mtu awe mvumilivu. Wengi wao wanaongea kifarsi tu. Bila kuwa na mkalimani isingewezekana.

Mama mkalimani ni mwislamu na mara nyingi anakutana na changamoto katika kutafsiri, hasa pale anapokutana na maneno ya kibiblia kama “sakramenti” au “utatu”. Lakini simulizi za kwenye Biblia zinawavutia wakimbizi kusimulia juu ya familia zao, jinsi ambavyo hawakuwa na uwezo wa kuagana na familia na marafiki zao. Wanasimulia juu ya hali walizokutana nazo katika kambi za wakimbizi, wasiwasi gani walio nao lakini hata juu ya nguvu wanayopata kupitia imani. Na ghafla maneno ya Yesu yanaanza kusikika:

“Na kila mtu aliyeacha nyumba, au ndugu wa kiume au wa kike, au baba, au mama, au watoto, au mashamba, kwa ajili ya jina langu, atapokea mara mia, na kuurithi uzima wa milele.”

Mathayo 19:29

Mistari kama huo ni uhasilia wa wakimbizi. Ghafla maneno mageni ya Yesu tunayaona mbele ya macho yetu yakitimia. Tunakutana na watu kwenye mazungumzo ambao maisha na imani ni zaidi ya tunavyoweza kufikiria. Tunaposikia habari ya muirani ambaye alikuwa akishiriki kwenye mikutana ya wakristo isiyokuwa halali, na kisha polisi walipowagundua, yeye akaruka kutokea dirishani ili asikamatwe. Au pale tunaposikia habari za mwanamke aliyemwagiwa tindikali na mume wake kisa alianza kuonesha kuvutiwa na dini ya kikristo. Katika hali hizi ndipo tunaelewa nini maana ya neema ya Mungu.

Mambo mengi wanayosimulia wakimbizi wa dini, yanavunja moyo. Lakini pia yanatufanya kuwaheshimu wakimbizi hasa kwa kuona uimara wa imani yao kwa Mungu. Pale tunapokutana nao basi pia tunajenga ukaribu nao, wanakuwa dada na kaka zetu katika imani. Wakimbizi hawasimami mbele yetu kama watakatifu, ila wanapata njia mioyoni mwetu pale wanaposimulia juu ya uzoefu, hofu, furaha na ukombozi wao kupitia injili. Kupitia kwao tunapokea ushuhudu wa Mungu na hata ujumbe wakitupa tumaini.

Mara nyingi kwenye vikundi vyetu, watu wamezoeana, hivyo hawaoni utofauti wa mila na desturi katika dini. Lakini utofauti huo upo na unaanza hata kwenye shule za watoto wadogo. Huko pia wanakutana watoto, wazazi na walezi wenye mitazamo tofauti. Ni muhimu kujadili namna tunaweza kufanikisha umoja baina ya watu wenye asili, mila na desturi tofauti. Katika kufanikisha hili lazima wazazi, walezi, walimu na watoto wawe tayari katika kushikiri katika mchakato wa kuimarisha umoja. Mchakato huu ni wa kudumu, na hivyo ni muhimu kujenga mazingira rafiki ya kuimarisha umoja huo.

Kwenye kazi za vijana, au elimu ya watu wazima na hata katika maeneo mengi ya kazi za kanisa, kanisa linahamasisha juu ya Ustadi wa Tamaduni na Desturi (*intercultural learning*). Mfano wa mchakato huu katika shule za chekechea na shule nyingine



Elimu ya uwingi katika vituo vya watoto

Vituo vya watoto vya kikanisa Altena, Iserlohn na Schwerte vinafata “mfumo wa pamoja “. Maana yake ni kwamba kila mtoto anapokelewa kama alivyo bila kujali anapotokea, lugha anayozungumza au asili aliyonayo. Wote wanaalikwa kushiriki na wanapokelewa. Kwenye chekechea hizo tatu wapo wafanyakazi waliohudhuria na kupata vyeti vya kozi ya Ustadi wa Tamaduni na Desturi na ambao wanazungumza kiingereza. Wanaelekezwa namna ya kutambua tofauti za kitamaduni kama vile namna ya kusalimiana, kuagaliana usoni wakat wa mazungumzo, au hata maswala ya kuzingatia muda.

Kufundishana mashuleni

Kuanzia 2016, katika shule ya Hans-Ehrenberg, wanafunzi kutoka mataifa saba wamekuwa wakijifunza kijerumani kwa pamoja. Uwezo wao wa lugha ukiwa mzuri ndipo wanaruhusiwa kushiriki katika madarasa mengine. “Kujifunza na kujua lugha kwetu maana yake ni kuishi pamoja, kujifunza juu za dini na tamaduni za kikristo”. Walimu mbalimbali na wafanyakazi wengine wa shule wanatoa kazi shirikishi katika kuwawezsha wanafunzi wa darasa hilo kuulewa utamaduni wa kikristo. Mfano ni kutengezea kwa mapambo ya Majilio na kuimba nyimbo za Krismas kwa pamoja. Kutoka shule ya rafiki Talitha Kumi huko Bethlehem/Palestina, shule ilipokea zawadi ya mfano wa zizi na hori la ngombe alipozaliwa Yesu. Zawadi hii inatumika kama chanzo cha mazungumzo na mijadala juu ya kuzaliwa kwa Yesu.

Katika mradi wetu wa „*Unsere Feiertage*“ (Siku kuu zetu), msisitizo unatolewa kwenye siku kuu mbalimbali ambazo ziko katika Kalenda. Tunayo interreligious calender darasani, ambayo inaonesha tamaduni za dini tofauti. Asili na maana ya tamaduni hizo zinaelezwa kwenye kalenda kwa kutumia alama au michoro. Tofauti na kufanana kwa tamaduni hizo kunajadiliwa darasani. Utofauti unaheshimiwa pia.

3.4 Kubeba majukumu



“Ninataka kufanya kazi yangu vizuri”

Halil Karacayli anaongoza Idara ya “Unterstütztes Wohnen Eckardtsheim” Bethel regional. Halil Karacayli alizaliwa Ujerumani, akiwa na miaka kumi yeye na familia yake walirudi nchini Uturuki. Akiwa huko alijifunza Kituruki na Kiarabu, lugha mama ya baba yake.

Mwaka 2004 ndipo alipoanza kufanya kazi Bethel regional. Mwanzoni alikuwa akifanya kazi na vijana wenye matatizo na sheria. “Baada ya miaka miwili katika kazi hiyo nilitakiwa kuiomba kazi hii upya. Wakati huo ndipo nilipogundua kuwa waombaji wa Kikristo walikuwa na nafasi kubwa ya kupata kazi kuliko mimi.” Licha ya kuwa yeye ni mualevi alipata hiyo kazi tena na sasa anaongoza idara, akiongoza watu 24. Kwa kulinganisha na idadi ya watu wanaofanyakazi Bethel, wafanyakazi 24 sio wengi maana Bethel inao wafanyakazi 19,000.

Je, Halil anafikiri dini yake itakuwa kikwazo katika maisha yake ya kazi? Inawezekana – au labda utakapotaka kuwa mkuu wa idara ngazi ya juu zaidi? “Haitakuwa rahisi, maana hakuna watu waliotangulia kushika nafasi hizo ambao sio wakristo.”

Je, kazi ya kuongoza idara inayotoa huduma za kidiakonia inakwendaje? “Wafanyakazi wenzangu hawapendi kuzungumzia jinsi kazi zao za kidiakonia zinavyoonekana kwenye maisha yao nje ya kazi. Ila mimi hupenda kuanzisha mada hii. Kila mtu anapendwa na Mungu. Ndio maana nasi inatupasa kuwapokea watu wote kwa upendo na heshima. Na hili, ndilo linawaainisha Wakristo na Waalevi kama mimi”

Je, zipo changamoto zinazozuia kuwepo kwa watu wenye asili tofauti katika mazingira yako ya kazi? “Nafikiri mafunzo ya huduma za kidiakonia yanatakiwa kufanyiwa mabadiliko ili hata watu wasio Wakristo wavutiwe na mafunzo hayo. Mabadiliko hayo yakifanyika, utofauti utakuwa sehemu ya Bethel huko mbeleni.”

Yesu anamtumia mtu mwenye imani tofauti kama mfano wa upendo anaotaka tuwape majirani zetu (Luka, 10:25.36). Tena msamaria haulizi juu ya utaiifa au dini, ila anamuonea huruma na anamsaidia mhitaji. Anakuwa jirani yake kwa kuwa anamuonea huruma na kumtendea wema. Tunasoma habari ya huruma katika Biblia pale Mungu anapoonza umaskini na taabu za watu (Mwanzo 16:13), pale anaposikia sauti na vilio vyao (Waamuzi 2,6-18), pale anapowakusanya waliotawanyika (Isaya 54:7). Lakini hata pale anapowaokoa, kuwasadia na hata kuwasamehe (Mika 7:18, Zaburi 103: 8). Huruma na haki hutegemeana; mtu mwenye huruma ni hakimu mzuri (Kutoka 23: 6). Huruma huleta haki kwa walioonewa (Walawi, Kutoka 20:20).

Migogoro ya kimataifa na ile ya bara la Ulaya kama mtikisiko wa uchumi wa 2008, mtikisiko wa uchumi wa Ugiriki wa 2015 na hata wimbi la wakimbizi viliambatana na changamoto kubwa. Hasa kwa utayari wa mtu binafsi wa kusaidia, uwezo wa taasisi za kiraia wa kuwakaribisha na kujenga umoja na wageni, uwezo wa kisiasa wa kukubaliana na changamoto hizo na utayari wa kuendelea kutii sheria na mikataba.



Kazi ya msingi ya Diakonia ni kuwahudumia na kuwasaidia wale ambao wanahitaji msaada lakini pia ambao mahitaji yao hayashughulikiwa kikamilifu na mfumo wa serikali wa kutoa hudumu za kijamii. Mara zote kazi za kidiakonia ni kumbusho, licha ya kuwa huduma zinazolenga kuwatoa watu kwenye dhiki lakini pia zinakumbusha umuhimu wa mabadiliko. Mabadiliko ili kupunguza vyanzo vya dhiki hizo.

Diakonie Austria, pamoja na Benz 2014

Changamoto kwa chama cha huduma ya kidiakonia

Mtu yeyote anayefanya kazi na watu wa asili na tamaduni tofauti anatakiwa kuwa “karibu na watu”. Ili kufanikisha hili wafanyakazi wanahitaji kuwa na ujuzi wa kuendesha mahusiano yenye watu wa tamaduni tofauti au wafanyakazi wenyewe wawe ni watu wenye asili ya uhamiaji na wenye ujuzi wa tamaduni na lugha tofauti. Kuna maeneo ya kazi ambayo tayari kuna uhaba wa wafanyakazi. Tayari upo umuhimu wa haraka kujua ni watu gani wanapaswa kufanya kazi katika taasisi za kanisa huko mbeleni.



Motisha yetu ya umoja wa kitamaduni (Interculturalism) sio kazi zinazohusisha tamaduni tofauti, bali ni ukosekenaji wa watu wa kujaza nafasi fulani za kazi. Kwa sasa kuna hitaji kubwa la nguvu kazi. Takribani nafasi 300,000 za kazi katika fani ya uuguzi nchini Ujerumani ziko wazi. Wako wakimbizi na watafuta hifadhi ambao wangependa kupata mafunzo katika sekta hiyo lakini sheria haziwapi haki hiyo. Lazima tujaribu kutafuta suluhisho la kisiasa ambalo litawawezesha watu walioko tayari kupata mafunzo kujaza hizo nafasi za kazi ambazo ziko wazi.

Mdiakonia Regine Buschmann, Idara ya Habari ya Bodelschwingschen Stiftungen Bethel

Hasa katika miji mikubwa ya Westfalia usahili wa wafanyakazi unakuwa wa mchanganyiko sana. Karibu theluthi moja ya watu wote wanaoishi Dortmund wana historia ya uhamiaji. Utofauti huu unaleta fursa mpya na ni faida kwa miji hiyo.

Idadi ya Waislamu pia inaongezeka. Mara nyingi watu wanaofanya kazi katika taasisi za kidiakonia ni Wakristo, tena washarika wa kanisa la Kikatoliki au wa kanisa la Kiinjili. Hata watu wanaojitolea wengi wao ni wa dini hizo. Kuwa na watu wenye asili tofauti ni muhimu katika vituo vya kidiakonia. Utofauti ni fursa nzuri kwa vituo vya kidiakonia.

Swali kuu ni Taasisi ya Diakonia kama muajiri inawezaje kulihakikisha hilo. Taasisi ya Diakonia inaongozwa kwa Sera ya Uaminifu wa Kanisa la Kiinjili la Ujerumani (EKD) kuhakikisha utendaji kazi wake unafata misingi ya kiinjili. Sera hizo zinaweka wazi sifa na viwango vinavyotakiwa kuzingatiwa wakati wa uteuzi wa wafanyakazi. Lengo kuu ni kuajiri watu ambao ni washarika wa moja ya makanisa chama ya EKD. Pia inawezekana kuajiri wafanyakazi kutoka kundi la kidini ambalo limo katika Chama cha Makanisa ya Kikristo (ACK). Kwa kufata vigezo maalumu, inawezekana pia kuajiri mtu ambaye sio mwanachama wa kanisa la Kikristo. Maombi ya watu ambao sio wanachama wa kanisa, yaani wale waliojiondoa katika kanisa hayazingatiwi.

Kutofautisha huku kunasaidia, tena kunaweza kuchangia katika kuleta uwazi wa kitamaduni katika taasisi za kidiakonia. Uwepo wa wahamiaji katika vikundi vya kazi unapelekea mabadiliko ya kijamii na kitamaduni kwenye mazingira ya kazi. Taasisi ya kidiakonia inaweza kujichafulia jina kama itawatenga na kutowapokea watu ambao wako tayari kuisaidia katika kutoa huduma.

Diakonia ingeficha utume wake na kujijeruhi yenyewe ikiwa ingewatenga watu ambao wako tayari kusaidia na kusaidia huduma yao. Soko la ajira la ujuzi linalozidi kuwa na ujuzi halina wafanyakazi wanaohitajika, soko hili pia ni mwanachama wa kanisa la Kiprotestanti. Ingekuwa ni lazima kuzingatia kanuni ya “wagombea wa kiinjili” basi vituo vingi vya Diakonisches Werk vingepaswa kufungwa. Soko la kazi (katika taasisi za kidiakonia) linahitaji watu wenye elimu sahihi ambao ni washarika wa kanisa la kiinjili. Lakini pia kama taasisi hizo zisingekuwa tayari kuajiri watu wasiokuwa Wakristo basi baadhi ya vituo vingefungwa kwa sababu ya kukosa nguvu kazi.



Mwaka 2016, Desemba Dortmund ilikuwa na wakazi 601,150; 104,115 walikuwa ni raia wa nchi nyingine. Hiyo ni asilimia 17,3 ya wakazi wa Dortmund. Kwenye wilaya kubwa kuliko zote Dortmund, yenye wakazi 59,648, 30,080 walikuwa na pasipoti ya kigeni, yaani asilimia 50,7.

Uwazi wa kitamaduni pia ni wa muhimu kwa sababu ya watu ambao huduma zetu za kidiakoni zinawalenga. Ikiwa, kwa mfano, unafanya kazi katika kituo cha usaidizi kwa watoto wenye ulemavu, unahitaji kujua ni uzoefu gani na maadili gani yanaathiri mazingira ya kitamaduni ya wazazi wa kituruki. Katika kazi, ujuzi wa tamaduni tofauti ni wa muhimu. Utofauti wa kitamaduni na asili inabidi uchukuliwe kama faida kwa mji na ofisi za serikali za mitaa. Serikali za mitaa pia zinatakiwa kuhakikisha muingiliano na mazungumzo ya tamaduni tofauti yanafanyika.

Muhimu zaidi ni kuwasaidia watu ambao maisha yao si bora, ambao hawana nafasi kushiriki katika mchakato wa kujenga umoja na wazawa. Bila nafasi ya ushirikiano, hofu na wasiwasi huongezeka kwa watu wasiokuwa na fursa sawa katika jamii. Taasisi za kidiakoni nazo zimetambua uwepo wa hofu na wasiwasi huo mfano katika kazi zake za kuwasaidia wasiokuwa na makazi na huduma za wakimbizi. Wafanyakazi wanapewa mafunzo maalumu ya usalama. Kupitia mafunzo hayo wafanyakazi wanajifunza jinsi ya kukabiliana na mashambulizi dhidi yao, mazingira ya ukatili na uhalifu. Mafunzo haya ni ya muhimu, maana katika utendaji kazi wafanyakazi hasa wa kike wanakutana na unyanyasaji. Unyanyasaji na wasiwasi wa kushambuliwa ni sababu kuu zinazotolewa na watu wanapoacha kazi.



Karibu Ulaya– Casa Copiilor in Dortmund.

Taarifa zaidi zinapatikana kwenye ukurasa wa facebook:
[www.facebook.com/diakoniedortmund/posts/
er%C3%B6ffnung-des-casa-copiilor-in/1872271163059770/](https://www.facebook.com/diakoniedortmund/posts/er%C3%B6ffnung-des-casa-copiilor-in/1872271163059770/)

4. Matokeo yake kwa Kanisa na Jamii

Sisi kama kanisa tunataka kuchangia kujenga jamii yenye watu wanaoishi pamoja vizuri na kwa amani. Lakini sisi kama kanisa pia tuna uzoefu ambao unaweza kutumika vizuri kwa manufaa ya jamii ambayo ina shida za uhamiaji. Uzoefu huu tunautoa katika kazi zetu za mahusiano na mawasiliano kati ya watu wenye dini tofauti; lakini hata katika kazi yetu ya Okumene. Pia kwa sababu ya uzoefu wetu katika masuala yahasuyo jamii, tunajitambua kama wadau wa serikali na taasisi za kijamii.

Sura hii inaelezea mambo au wajibu wetu sisi, kanisa la kiinjili la Westfalia. Sura hii pia inaongelea madai yetu dhidi ya serikali na misimamo yetu tunayotakiwa kuiingiza katika mijadala ya kisiasa na kijamii.

4.1 Kuimarisha mazungumzo – Kukuza maendeleo ya kitamaduni ya kanisa

Kuimarisha mazungumzo

Mkristo anayeishi Ujerumani sasa haonekani mara nyingi kwenda kwenye ushrika wake. Ujerumani yapo makundi mbalimbali ya kidini na watu wanaoishi kwa imani tofautitofauti. Kwa sababu hizi inakuwa vigumu kuwa na mazingira kwenye sharika ambazo zinakutanisha washarika na watu wa madhehebu mengine kushiriki katika mazungumzo ya kiokumene. Sharika na Jumuiya ya Kazi za Makanisa (ACK) zinatambua uwepo wa hayo makundi ya Wakristo, Freikirchen na sharika ambazo zinaundwa na wahamiaji; lakini si mara zote kumekuwa na uhusiano mzuri nao, na yapo makundi ya Kikristo ambayo hayataki uhusiano huo.

Wahamiaji wengi waliofika Ujerumani wametokea nchi ambapo wananchi wengi si Wakristo. Waislamu kutoka makundi tofauti, Wayahudi, Wahindu, Wabuda, Waaelewi, Wabaha, Kasalinga na watu wa dini nyingine wamehamia Rhein Kaskazini-Westfalia na mara nyingi wanajumuika na wenzao ambao wameshakuwa wenyeji huku. Hasa jumuiya za Kiislamu zinaweza kuwasaidia wahamiaji wengi. Ikumbukwe kuwa matumizi ya lugha za kigeni tu, au kujumuika na watu wa kabila au asili moja kunaweza kuwa changamoto kwa mchakato wa kufanikisha kuchanganyikana na kuisha kwa umoja kati ya wenyeji na wageni.

Mazungumzo ya muondoko wa pamoja wa dini yanagusa udini wa wahamiaji na unalenga kuwawezesha kufurahia haki yao ya uhuru wa dini. Kupitia mazungumzo ya muondoko wa pamoja wa dini, wageni wanapata taarifa za siku kuu za kidini au namna ya kupata mahali pa kusalia kwenye mahospitali. Kupitia mikutano ya watu wa dini tofauti na madhehebu tofauti, umoja wa jamii unastawi.

Kwa waumini wa dini kuu za hapa Ujerumani mazungumzo ya muondoko wa pamoja wa dini ni ya muhimu sana maana mazungumzo na waumini wa dini au madhehebu tofauti kunawasaidia kujiainisha. Ipo mifano mizuri ya matukio yanayoandaliwa na dini na madhehebu tofauti kama maombi ya amani ya dini zote, wiki za kusherehekea mila na desturi tofauti zilizopo Rhein Kaskazini-Westfalia na wiki za kushereheka undugu.

Mazungumzo ya muondoko wa pamoja wa dini yana historia ndefu Rhein Kaskazini-Westfalia. Kuanzia miongo iliyopita, mahusiano ya dini na madhehebu yamekuwa yakitunzwa kwa heshima na kuaminiana. Kwa misingi hiyo dini na madhehebu tofauti kwa pamoja zimekuwa zikikabiliana na changamoto za kidini, kibinadamu, kisiasa na kijamii kwa pamoja.

Kukuza utofauti wa asili ndani ya kanisa

Utofauti (wa dini, asili, muonekano n.k.) ni zawadi ambayo inatakiwa kutunzwa. Hata utofauti wa watu, kwa mila na desturi na asili nao ni wa muhimu tena unaweza kuwa wa faida kubwa kwa kanisa letu.

Katika utekelezaji wa kufaidi zawadi hii ya utofauti, sharika zinaweza kuanzisha mijadala na wahamiaji. Mijadala hii ilenge kutoa nafasi ya kufahamiana na kujadili kwa pamoja njia za kuweza kuwahusisha wahamiaji katika maisha na ratiba za sharika husika. Hili ni rahisi kufanyika hasa na wahamiaji ambao tayari wana mahusiano na usharika kupitia vituo vya watoto wadogo na vijana au hata sehemu nyingine za usharika. Presbyteries zinasanifu mkakati wa kukuza utofauti katika kamati za kanisa. Na mikakati hiyo inajenga sehemu ya dhana ya sharika na itatekelezwa hatua kwa hatua

Majimbo nayo yanajihusisha na mada hii kwenye mikutano ya majimbo pamoja na kujiuliza ni katika kamati zipi utofauti wa mila na desturi pamoja na ule wa asili unaweza kuwa wa faida. Nao wanasanifu mikakati ya namna ya kuutumia huo utofauti. Mikakati hiyo nayo inakuwa sehemu ya dhana ya majimbo.

Hatimaye kanisa linapitisha mkakati wa kuutumia huo utofauti kwa manufaa ya kanisa kwa ujumla. Mkakati huo unazingatiwa katika dhana ya maendeleo ya wafanyakazi, ukuzi wa kazi za hiari na unafanyika kwa misingi ya *Diversity Management*.



Nimefurahi sana kuona kwamba kanisa la kiinjili linatambua haja ya kuwa wazi na tayari kupokea watu wa asili na mila na desturi tofauti. [...] Utayari wa kupokea tamaduni tofauti katika taasisi binafsi, mifumo ya serikalina mamlaka za serikali ni suala muhimu sana kwangu. Uwazi wa kitamaduni ni muhimu ili kuwawezesha watu wenye historia ya uhamiaji kufika na kuwa sehemu ya jamii zetu. Lakini pia utayari na uwazi huu ni muhimu katika sekta za kibiashara na kiuchumi ambazo hadi sasa zimekuwa zikipungukiwa nguvu kazi. Wahamiaji wanaokuja na sifa na ujuzi wanaweza kujaza nafasi hizo, hivyo ni muhimu kufanya mabadiliko katika sekta hizo ili nguvu kazi tulizozipata kupitia wahamiaji zitumike.

Serap Güler, Integration Secretary katika Wizara ya Watoto, Familia, Wakimbizi na Integration ya Jimbo la Rhein Kaskazini-Westfalia

4.2 Kutoa hifadhi ya Kanisa – Kusisitua haki ya kupata Asylum – kuhakikisha njia salama

Kutoa hifadhi ya kanisa

Maana ya “Hifadhi ya kanisa” ni pale mkimbizi anapopewa hifadhi ya usharika, ili vyombo vya serikali visimrudishe mkimbizi huyo alikotoka. Idadi ya watu waliopewa hifadhi ya kanisa ni ndogo pale inapoliganishwa na idadi ya wakimbizi waliofika Ujerumani. Inasemekana kuanzia mwaka 2010 tumepokea zaidi ya wakimbizi milioni moja. Jumuiya ya kiokumene iitwayo Bundesarbeitsgemeinschaft Asylum in der Kirche imetoa taarifa kuwa hadi Novemba 2017 idadi ya watu waliopewa hifadhi ya kanisa walikuwa 348, wakati Wizara ya Uhamiaji na Wakimbizi hadi Novemba 2017 ikiripoti idadi ya watu waliopewa hifadhi ya kanisa kuwa 679. Hadi September mwaka huo, Rhein Kaskazini-Westfalia jumla ya hifadhi ya kanisa zilikuwa 100.

Licha ya idadi ya hifadhi za kanisa kuwa chini bado hifadhi hii huleta utata. Wapo wanaodai kuwa hifadhi ya kanisa ni hifadhi ambayo hukiuka mipaka ya taratibu na sheria za nchi, na kuwa inaweka utu mbele ya sheria na hivyo kupelekea kudidimia kwa utawala wa sheria. Ukweli wa hoja hizi ni kwamba hifadhi ya kanisa husitisha kurudishwa kwa wahamiaji nchini kwao. Lakini hifadhi hii haitolewi kihorelahorela na wala sio hatua inayopinga taratibu za serikali. Hifadhi ya kanisa ni huduma ya kiroho na kidiakonia kwa wahitaji. Dhumuni ni kutoa nafasi mpya ya mazungumzo kati ya serikali na mkimbizi kwa kusindikizwa na kanisa. Makanisa yanatoa hifadhi kwa wakimbizi, yanakuwa yanaona kuwa hiyo ndiyo nafasi yake ya mwisho, ili mkimbizi huyo asirudishwe alikotoka ambako labda anaweza akateswa na maisha yake kuwa hatarini.

Serikali inaheshimu hatua hii ya kanisa na ndio maana mwaka 2015, Kanisa na Wizara ya Uhamiaji na Wakimbizi zilikubaliana juu ya taratibu za kesi maalumu za wakimbizi. Kwa makubaliano hayo serikali haingilii kati pale mkimbizi anapopewa hifadhi ya kanisa bali inakubali kutokomrejesha nchi aliyotoka na kupitia tena maamuzi ya awali kwa mkimbizi husika. Ila pia kanisa linatakiwa kuwasiliana na wizara juu ya uwepo wa kila kesi ya hifadhi ya kanisa. Hifadhi ya kanisa sio hatua inayochukuliwa na kanisa kwa maficho, bali kuna makubaliano na serikali.

Kesi nyingi za hifadhi ya kanisa, baada ya 2005 ziliamuliwa upya kwa manufaa ya wakimbizi. Wakimbizi walihakikishiwa haki ya kuendelea kubaki Ujerumani

Kuimarisha haki ya ukimbizi na maisha bora katika nchi nyingine kwa ajili ya kuepokana na udhalimu (the right to asylum)

Kwenye Azimio la Ulaya juu ya haki za binadamu na Mkataba wa Haki za msingi wa Umoja wa Ulaya zinataja haki za wakimbizi ambazo hazipishani na zile ambazo ziko kwenye Mkataba wa kimataifa wa haki ya wakimbizi. Nchi zote ambazo zimeridhia na kusaini Mkataba huo zinatakiwa kuwapa wakimbizi hifadhi na kukakisha maombi yao ya kuendelea kubaki katika nchi hizo yanazingatia taratibu na sheria.

Kwa bahati mbaya kwenye nchi za umoja wa ulaya hakuna maendeleo mazuri, katika kuhakikisha kuwa nchi zote za umoja wa huo zinakidhi viwango sawa katika kutoa haki ya ukimbizi, kubaki na maisha bora kwa wakimbizi. Hata haki ya wakimbizi, kushiriki katika fursa za kijamii katika nchi nyingi za Ulaya sio hakika. Nchi ambazo zina mipaka yake ndiyo ukomo wa mipaka ya Ulaya, hasa nchi za Ulaya ya Kati, kusini na Mashariki huwazuia wakimbizi kuingia kuwasili katika nchi hizo. Wakimbizi wanaofanikiwa kuvuka mipaka hawapati hifadhi na hupewa huduma ambazo sio za kuridhisha. Kutokana na ulinzi mkali uliopo kwenye mipaka ya nchi hizo, wakimbizi wengi hushindwa kuingia na kuomba hifadhi. Hatua hii ni kinyume na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Wakimbizi. Inasikitisha kuwa tumefikia hatua ambapo meli zinazokuwa zimebeba wakimbizi waliookolewa baharini kuzuliwa kutia nanga katika nchi hizo.

Kwa kulinganisha na nchi nyingi, Ujerumani ina viwango vya juu kwenye huduma wanazopewa wakimbizi. Hata hivyo serikali ya Ujerumani inachangia katika kutekeleza sera ya kujitenga kwa bara la Ulaya. Kwa mfano kwenye „*Asylpaketen*“ na katika Sheria ya Utekelezaji wa kuondolewa kwenye eneo la nchi ya Ujerumani (Gesetz zur Durchsetzung der Ausreisepflicht) vipo vifungu vingi ambavyo makusudi yake ni kutishia wakimbizi na kwa namna moja au nyingine haviendani na makubaliono yalipo kwenye Mkataba wa kimataifa wa haki za wakimbizi..

Kanisa la Kiinjili la Westfalia linapinga kifungu kinachotamka kuwa wakimbizi ambao wamefanya maombi yao rasmi na kupata hifadi wanaweza kutakiwa kubaki kwenye kambi za wakimbizi kwa kipindi cha miezi 24 au zaidi. Ndani ya huo muda wakimbizi hawana haki ya kuhudhuria mafunzo ya mshikamano, ajira na watoto sio lazima waende shule.

Lakini pia kuna changamoto katika kutambua uwepo wa wakimbizi wenye matatizo ya kisaikolojia na magonwja mengine hasa yaliyotokana na hali ya ukimbizi. Pia kimaadili na kisheria inashangaza kuona kwamba wakimbizi wenye “subsidiary proteccion” wananyimwa haki ya kuleta familia zao. Taratibu hizi ni kinyume na haki ya msingi ya kulinda ndoa na Familia na Mkataba wa kimataifa juu ya haki za wototo.

Sisi kama kanisa hatutakaa kimya kuhusu maswala haya, tutaendelea kupaza sauti na kuweka wazi kuwa njia sahihi ni kuwa na sera ya yenye utu kwa wakimbizi katika nchi zote za Ulaya.

Kuhakikisha uwepo wa njia salama

Kama chombo cha ziada, EKVW inataka kuwepo na njia salama za wakimbizi wenye haki ya kupewa hifadhi kufika Ujerumani. Nchini Italia tayari kuna programu hizo. Mfano ni “Ukanda ya kibinadamu” (Humanitarian Corridor). Hii ni programu ambayo ilizinduliwa mwaka 2015, ikiwa ni ushirikiano baina ya shirika la kiokumene la kiprotestanti linaloitwa “Mediterranean Hope”, Jumuiya ya Sant’Egidio na Serikali ya Italia. Synod ya kanisa la Westfalia imetamka utayari wake wa kuanza mradi wa majaribio kwa ajili ya wakimbizi 100, kwa kushirikiana na wadau wengine, hasa makanisa mengine ya Rhein Kaskazini-Westfalia pamoja na Kanisa la Kiinjili la Ujerumani wapo katika mazungumzo na Wizara ya Mambo ya Ndani ili programu kama hizi zitekelezwe hata Ujerumani nzima. Hadi sasa tunaona kuna uwezekano wa mradi wa Community Sponsorship-Pilotprojekts (CSP) kutumika katika kuboresha programu ya makazi mapya (Resettlement-Programm) ya serikali.



Mediterranean Hope ni shirika la kuhudumia wakimbizi linalomilikiwa na makanisa tunayoshirikiana nayo ya nchini Italia. Makanisa ni ya waldesians na wamethodist. Kupitia mradi wa “Humanitarian Corridor” watu 1,000 wenye kuhitaji ulinzi na hifadhi maalumu wameweza kupata viza ya kibinaadamu (humanitarian visa) ya kutoka Libanon na kufika Italia. Baada ya kufika, kanisa liligharamikia na kuhakikisha watu hao wanapata huduma muhimu wakati wa kusubiri maamuzi juu ya maombi yao ya hifadhi. Pia Kanisa Katoliki nalo limejitokeza kushiriki katika programu hiyo, kwa kutaka kuwasadia wakimbizi kutoka Sudan. Mipango ya kuwa na mradi huo kwa ajili ya wakimbizi waliako Morroko nayo imekamilika. Nchini Ufaransa na Ubelgiji nako kuna miradi inayofanana na huu mradi. Makubaliano baina ya makanisa na serikali yamekamilika.

4.3 Kupitisha sheria ya uhamiaji

Tunaona umuhimu wa kuwepo kwa sheria ya uhamiaji, na muda umefika wa serikali ya Ujerumani kufikia muafaka juu ya sheria hiyo. Ili kufanikisha umoja baina ya wazawa na wahamiaji ni lazima kuwepo na mkakati endelevu wa uhamiaji. Mkakati huo lazima uwe na malengo mahsusi.

Mpango huo lazima uzingatie utu na ulenge kuboresha maisha ya wazawa na wahamiaji. Uwepo wa sheria ya uhamiaji ni ishara ya serikali kutambua kuwa Ujerumani ni nchi yenye kupokea wahamiaji (immigration country). Pia itakuwa ni ishara ya kuwatambua wahamiaji pamoja na tofauti zao, na kuonesha kuwa hilo lina manufaa kwa jamii nzima. Sheria hiyo pia inaweza kurahisisha upatikanaji wa nguvu kazi, maana sheria hiyo inaweza kuweka wazi taratibu na sifa za kufuatwa ili mtu ahamie Ujerumani na kufanya kazi.

Sheria hiyo lazima itungwe kwa kuzingatia misingi za haki za binadami bila kusahau haki za wakimbizi kama zinavyoelezwa kwenye Mkataba wa kimatafiafa ya haki za wakimbizi. Sheria hiyo lazima ilenge kurahisisha taratibu za kuhamia Ujerumani pamoja na kutoa muongozo wa kufanikisha umoja wa wazawa na wahamiaji. Muhimu pia, sheria hiyo ni lazima itoe haki sawa kwa wakimbizi na wahamiaji.



Maamuzi muhimu (key decision) ya namna ya kuwapokea wakimbizi yaliamuliwa kutoka ngazi za juu na kusambazwa katika ngazi za chini. Mabadiliko katika jamii ya uhamiaji (jamii yenye kupokea wahamiaji) yanaweza tu kufanikiwa kama maamuzi yote yatafikiwa kidemokrasia, kuanzia ngazi za chini kwenda juu.

Markus Langer, Mkurugenzi Mkuu wa Brand Communication, Evonik Industries AG

4.4 Kusimamia misingi muhimu

Hadhi na thamani ya kila mwanadamu ni ya kudumu

Kila binadamu ameumbwa kwa mfano wa Mungu, hivyo watu wote tunatakiwa kuonesha hadhi na thamani kwa binadamu wenzetu. Sisi, Kanisa la kiinjili la Westfalia, tunaajihusisha na kutetea haki za binadamu tunasisitiza Umoja wa Ulaya kuwa na sera ambazo hazipishani na misingi ya haki za binadamu na sheria za kimataifa za haki za binadamu. Licha ya hayo tunaendelea kuhimiza na kuisistiza juu ya haki za wakimbizi, wahamiaji na watu wenye asili ya uhamiaji. Muhimu wote wawe na haki sawa, fursa sawa ili kuweza kuboresha maisha ya kila mtu na jamii kwa ujumla.

Umoja ndio ufunguo wa mabadiliko katika jamii

Kuna changamoto zilizoibuka, baada ya kuanza kutekeleza jukumu la kuhakikisha kuwa wahamiaji wanapata fursa sawa na wazawa, pamoja na kuwafanya sehemu ya jamii. Kimsingi changamoto hizi sio ngeni, ni changamoto ambazo zina mizizi katika jamii yetu. Changamoto hizo zilitakiwa kuwa zimepatiwa ufumbuzi siku nyingi.

Viwango vya umaskini nchini Ujerumani bado viko juu. Mwaka 2017 watu 16% ya wananchi walikuwa maskini. Hata watu ambao wana kazi bado wanaishi katika hali duni. Hasa familia zenye watoto wengi, mzazi mmoja, watu wenye asili ya uhamiaji na wastaafu ndizo zinazoishi katika umaskini. Mpaka sasa watoto wanaoishi kwenye umasikini wamefikia 19%. Kwenye miji mikubwa katika eneo la Ruhr idadi ya watu watu waishio kwenye umaskini imefika hadi 50%. Pamoja na hayo mafanikio kielimu yana uhusiano mkubwa na nafasi yake katika jamii. Hali ya watu kutengwa au kujisikia kutengwa na jamii inaongezeka. Hata kupata nyumba ya bei nafuu ni vigumu, sababu moja ikiwa ni uzembe katika kuendeleza na kudhibiti sekta ya makazi.

Matatizo haya ni ya siku nyingi, lakini sasa wakimbizi wanasingiziwa kuwa wao ni chanzo cha matatizo haya. Makundi (tena wakati mwingi ni makundi ya watu wenye asili ya uhamiaji) ndani ya jamii yanaeneza ubaguzi wa rangi, wivu wa kimaendeleo dhidi ya wakimbizi. Matatizo mengi (mfano ukosefu wa nyumba za bei nafuu za kupanga kwa ajili ya wasiokuwa na makazi au watu wenye magonjwa ya akili) yanaongezeka kwa sababu wazawa na wahamiaji wote wanapigania nafasi chache zilizopo.

Ndio maana kuna haja ya kuwa na sera ambazo zinalenga kuimarisha umoja na kuhakikisha kuwa wahitaji, wazawa kwa wahamiaji wanapewa huduma wanazohitaji. Taasisi zinazohusika na kujenga makazi na kupanga mji zinatakiwa kuzingatia mahitaji ya wazawa na wahamiaji bila kuwasahau wakimbizi. Lazima kuwepo na mkakati wa kuwezesha umoja wa wazawa na wahamiaji utakao tekelezwa ngazi ya taifa, majimbo na serikali za mitaa.

Mkakati huo lazima ulenge upanuzi wa makazi ya kijamii, uwepo wa mfumo wa elimu wa ushirikiano na si wa kutofautiana, hatua za kukuza maisha ya familia kwa kutoa haki za wakimbizi kuleta familia zao na kupambana na umasikini wa watoto. Lakini pia mkakati huo lazima uzingatie kuendelezwa kwa maeneo duni ya miji na haki sawa katika soko la ajira bila kujali asili ya mtu. Sera yenye kugusia maeneo hayo, inaweza kuwa ndio ufunguo wa mabadiliko ya kijamii.

Kukabiliana na makundi ya mrenge mkali wa kulia

Wasiwasi wa baadhi ya watu unaotokana na mabadiliko yanayoletwa uhamiaji unawafanya badhi ya watu kujitenga na jamii. Wasiwasi na maoni yao lazima yazingatiwe na kuchukuliwa kwa uzito.

Chuki dhidi ya wageni na ubaguzi wa rangi hata kanisani upo. Ndio maana ni muhimu kanisa kuwalinda watu wote dhidi ya unyanyasaji na chuki hizo. Lazima kanisa litoe matamko yakupinga chuki dhidi ya wakimbizi, wayahudi, uchochezi na ubaguzi wa rangi. Makanisa yana nafasi kubwa katika kuhakikisha maswala yanayowasumbua na kuwagusa wazawa na wakimbizi yanapewa nafasi katika mijdala ya umma na siasa. Matatizo mengine ya kijamii kama vile umasikini, ubaguzi ni lazima yawekwe wazi ili kutafutiwa suluhisho.

Sharika zina nafasi ambazo zinaweza kutumika kwa ajili ya mawasiliano na mazungumzo ya wazi, nafasi hizo pia zinaweza kutumika kwa ajili ya majadiliano juu ya changamoto ambazo jamii inakabiliana nazo. Kwa kutumia nafasi hizo watu wanatakiwa sio tu kuzungumza juu ya imani zao bali hata hofu zao na wasiwasi wao. Kanisa lazima liwe ni eneo ambapo watu wako huru kutoa mawazo yoa. Muhimu zaidi lazima kanisa litambuliwe kuwa eneo ambapo watu wenye mitazamo tofauti wanaweza kushiriki kwenye majadiliano na kuheshimiana.

Muhimu pia ni nafasi za kielimu zinazochangia kukuza demokrasia ambazo hutelewa kwenye sharika kwa ajili ya makundi mbalimbali ya jamii. Mfano shule za awali na kazi za vijana, mashule, nafasi za kujiendeleza kwa ajili ya watu wazima na vikundi vya akina baba na mama nk. Zaidi ya hayo ni muhimu kukuza ustadi wa mila na desturi tofauti tofauti wa wafanyakazi wa kanisa.

Hitimisho

“Nilikuwa mgeni nanyi mkanikaribisha” Sisi Kanisa la Kiinjili la Westfalia tunaamini neno hili la Yesu ni la muhimu sana nyakati hizi

Watu hutofautiana kwa sababu hata uumbaji wa Mungu ni wa rangi nyingi na namna mbalimbali. Kwa sababu ya kuumbwa tofauti, ndio maana wanadamu hutofautiana katika mambo mengi, kutofautiana huko huonekana hata katika mazungumzo, mijadala na mitazamo.

Watu wanategemeana, wanachukuliana, na sababu kuu ya kuishi kwao ni kukubaliwa na Mungu kama walivyo. Tukiishi hivi maisha bora na mazuri yanaweza kupata nafasi katika jamii zetu.

Tunapokutana na wakimbizi wenye njaa na kiu, walio uchi, wafungwa, wasiokuwa na makazi na waliopotea tunakumbushwa kushindwa kwetu, na hata dhambi zetu. Tunapokutana na wahitaji tunakutana pia Krisito mwenyewe. Yesu Kristo anatumkumbusha kujirudi na kuishi maisha yanayolitukuza jina lake.

Wito huu wa kujirudi unatakiwa kuongezeka hasa pale watu wengi wanapoanza kushindana na kubishana kwa propaganda na vurugu. Tunatambua pia kuwa hali ya watu kujitenga na wale wawaoonao kama “marafiki” na “maadui” inaendelea kuongezeka.

Kupitia toleo hili ambalo linaufikia umma “public” tunataka kuwatia moyo watu na kuwahamasisha. Hasa, tunalenga kuwahamasisha na kuwatia moyo wale ambao wanakutana na changamoto nyingi katika kazi zao za kuleta maridhiano na upatanishi. Hivyo basi, ni muhimu kumpa mkono yule anayezama, kumpa sauti aliyenyamazishwa na kuwapa haki zao wale walioonewa. Lengo ni kujenga mazingira ambamo vyanzo vya matatizo ya binadamu vinaweza kupungua au hata kutokomezwa. Vile vile ni lazima kutoa misaada maalumu kwa wahitaji bila kutumia sheria kama kisingizio cha kutotoa misaada hiyo. Sambamba na hilo ni lazima kuutambua na kuukubali utofauti wa watu kwenye jamii yetu ya uhamiaji. Tunatakiwa kukubaliana kuwa nchi yetu ni nchi ya wahamiaji.

Tunataka kujenga mazingira ambamo kila mwanajamii ataweza kujisikia kuwa ni sehemu ya jamii yetu na anaweza kufaidi fursa ambazo jamii yetu inazitoa. Tunataka kukuza ushirikiano katika jamii yetu. Na kama ilivyotajwa hapo awali, utayari wa kuchukuliana ni mchakato wa pande zote mbili. Ni mchakato wa pamoja wa wazawa na wageni.

Tunatambua kuwa sisi wakristo tunashindwa (sasa na hata nyakati za nyuma) katika kutimiza wajibu huu. Wito wa kujirudi na kumrudia Mungu unatulenga sisi wenyewe. Tuko pamoja na wale wote wanaochukua hatua kuelekea maisha yenye kufurahia utofauti ndani ya jamii. Pamoja na wao tunataka kuikabili changamoto itokayo kwa Kristo mwenyewe:

“Nilikuwa mgeni nanyi mkanikaribisha.”

Waliochangia katika kufanikisha kwa toleo hili ni:

Prof. Dr. Dieter Beese
Landeskirchenrat,
Evangelische Kirche von Westfalen

Dr. Michael Bertrams
Mitglied der Kirchenleitung,
Evangelische Kirche von Westfalen

Christina Biere
MÖWe-Regionalpfarrerin
für die Kirchenkreise Dortmund, Hagen,
Hattingen-Witten und Schwelm

Christian Binder
Pfarrer im Fachbereich Gottesdienst
und Kirchenmusik, Institut für Aus-,
Fort- und Weiterbildung der
Evangelischen Kirche von Westfalen

Monsignore Dr. Michael Bredeck
Priester und Leiter der Zentralabteilung
Entwicklung, Erzbischöfliches Generalvikariat
des Erzbistums Paderborn

Klaus Breyer
Pfarrer und Leiter des Instituts
für Kirche und Gesellschaft der
Evangelischen Kirche von Westfalen

Prof. Dr. Martin Büscher
stellvertretender Institutsdirektor, Rektor der
Kirchlichen Hochschule Wuppertal / Bethel

Prof. Dr. Mark Burrows
Dozent für Gemeindepädagogik
und Diakonie, Evangelische Hochschule
Rheinland-Westfalen-Lippe

Prof. Dr. Klara Butting
Leiterin des Zentrums für biblische Spiritualität
und gesellschaftliche Verantwortung
an der Woltersburger Mühle

Elsie Joy de la Cruz
Pfarrerinnen im Evangelischen Kirchenkreis Vlotho

Carmen Damerow
Dezernat 22: Weltmission, Ökumene
und kirchliche Weltverantwortung,
Evangelische Kirche von Westfalen

Dr. Jan-Dirk Döhling
Kirchenrat, Dezernent für gesellschaftliche
Verantwortung, Evangelische Kirche von Westfalen

Dietrich Eckeberg
Referent und Geschäftsführer des Fachverbandes
Migration und Flucht, Diakonisches
Werk Rheinland-Westfalen-Lippe

Martina Espelöer
Superintendentin,
Evangelischer Kirchenkreis Iserlohn

Dirk Gellesch
Mitglied der Kirchenleitung,
Evangelische Kirche von Westfalen

Jens Hansen
Pfarrer und Mitglied der Kirchenleitung;
Waldenserkirche in Italien

Dr. Thomas Heinrich
Landeskirchenrat,
Evangelische Kirche von Westfalen

Albert Henz
Theologischer Vizepräsident i. R.,
Evangelische Kirche von Westfalen

Beate Heßler
Pfarrerinnen, Fachstelle Gemeinsam Kirche sein
und Ökumenische Frauenarbeit, Amt für Mission,
Ökumene und kirchliche Weltverantwortung
der Evangelischen Kirche von Westfalen

Gerd-Matthias Hoeffchen
Chefredakteur, Unsere Kirche

Helge Hohmann
Pfarrerinnen und Beauftragter
für Zuwanderungsarbeit der Evangelischen Kirche
von Westfalen, Institut für Kirche und Gesellschaft
der Evangelischen Kirche von Westfalen

Wolfgang Hüllstrung
Pfarrer, Evangelische Kirche im Rheinland

Prof. Dr. Traugott Jähnichen
Dozent für Christliche Gesellschaftslehre,
Ruhr-Universität Bochum

Dirk Johnen
Redakteur, Amt für Mission, Ökumene
und kirchliche Weltverantwortung der
Evangelischen Kirche von Westfalen

Christa Kronshage
Mitglied der Kirchenleitung,
Evangelische Kirche von Westfalen

Ralf Lange-Sonntag
Theologischer Referent für die Bereiche
„Weltreligionen, insbesondere Islam“ sowie
„Mittlerer und Naher Osten“ im Landeskirchenamt,
Evangelische Kirche von Westfalen sowie
Fachstelle „Christlich-islamischer und
interreligiöser Dialog“ im Amt für Mission,
Ökumene und kirchliche Weltverantwortung

Christoph Lindemann
Stabsstelle Kommunikation,
Evangelische Kirche von Westfalen

Dr. Ulrich Möller
Oberkirchenrat, Dezernent für Weltmission,
Ökumene und kirchliche Weltverantwortung
Evangelische Kirche von Westfalen

Annette Muhr-Nelson
Pfarrerin und Leiterin des Amtes für Mission,
Ökumene und kirchliche Weltverantwortung
der Evangelischen Kirche von Westfalen

Dr. Jean Gottfried Mutombo
MÖWe-Regionalpfarrer für die
Kirchenkreise Unna, Hamm, Münster,
Steinfurt-Coesfeld-Borken und Tecklenburg

Prof. Dr. Alexander-Kenneth Nagel
Geschäftsführender Direktor und
Dozent am Institut für Soziologie
der Sozialwissenschaftlichen Fakultät,
Georg-August-Universität Göttingen

Ingo Nesperke
Pfarrer und Leiter des Instituts für
Gemeindeentwicklung und missionarische Dienste

Doris Peschke
Referentin – Projektleitung „Wege in die Legalität“
Diakonisches Werk in Hessen und Nassau
und Kurhessen-Waldeck e.V.

Anne Rabenschlag
Geschäftsführerin, Diakonisches Werk
Dortmund und Lünen gGmbH

Prof. Dr. Gerhard K. Schäfer
Rektor a.D., Evangelische Hochschule
Rheinland-Westfalen-Lippe

Mehrdad Sepehri Fard
Pastor in der Projektstelle „Seelsorge für
persischsprachige Christinnen und Christen“
der Evangelischen Kirche von Westfalen

Prof. Dr. Michael Welker
Geschäftsführender Direktor des
Forschungszentrum Internationale
und Interdisziplinäre Theologie (FIIT),
Universität Heidelberg

Dr. Katalina Tahaafe-Williams
Programmreferentin für Mission
und Evangelisation, Ökumenischer Rat der Kirchen

Prof. Dr. Peter Wick
Lehrstuhl für Exegese und Theologie
des Neuen Testaments, Geschichte des
Urchristentums an der Evangelisch-Theologischen
Fakultät der Ruhr-Universität Bochum

Birgit Worms-Nigmann
Pfarrerin und Mitglied der Kirchenleitung,
Evangelische Lydia-Kirchengemeinde Dortmund

Dr. Claudia Währisch-Oblau
Pfarrerin, Leiterin der Abteilung Evangelisation,
Vereinte Evangelische Mission

Vyanzo:

Asyl in der Kirche (o. J.): **20 Jahre Asyl in der Kirche.** Eine dokumentarische Ausstellung. Ein Leitfaden zum Rundgang durch die Wanderausstellung.

URL: www.kirchenasyl.de

Bade, Klaus J. (2017): **Migration – Flucht – Integration.** Kritische Politikbegleitung von der „Gastarbeiterfrage“ bis zur „Flüchtlingskrise“. Erinnerungen und Beiträge

URL: www.imis.uni-osnabrueck.de/fileadmin/4_Publikationen/PDFs/Bade_Migration.pdf [11. Juli 2017]

Baumann, Martin (2004): **Religion und ihre Bedeutung für Migranten.** Zur Parallelität von „fremd“-religiöser Loyalität und gesellschaftlicher Integration.

In: Beauftragte der Bundesregierung für Migration, Flüchtlinge und Integration (Hrsg.): Religion – Migration – Integration in Wissenschaft, Politik und Gesellschaft. Berlin, Seiten 19–30

Beese, Dieter: **Barmherzigkeit**

In: Friedrich, Norbert u.a. (Hrsg.): Diakonie-Lexikon. Göttingen 2016, Seiten 46–49

Benz, Benjamin: **Armenhilfepolitik. Soziale Arbeit als „Hilfe unter Protest“ am Beispiel der Tafeln.**

In: Ders. u. a. (Hrsg.), Politik Sozialer Arbeit, Band 2: Akteure, Handlungsfelder und Methoden. Weinheim 2014, Seiten 122–140

Brot für die Welt –
Evangelischer Entwicklungsdienst (2017):
Flucht(ursachen)bekämpfung.

Standpunktpapier. Berlin

Bundesamt für Migration und Flüchtlinge (BAMF) (2016): **Wanderungsmonitoring: Erwerbsmigration nach Deutschland.** Jahresbericht 2015.

URL: <http://www.bamf.de/SharedDocs/Anlagen/DE/Publikationen/Broschueren/wanderungsmonitoring-2015.pdf> [21. Juli 2017]

Bundesverwaltungsamt (BVA) (o.J.): **Spätaussiedler und ihre Angehörigen.** Zeitreihe 1992–2015. Herkunftsstaaten – ehemalige Sowjetunion.

URL: www.bva.bund.de/SharedDocs/Downloads/DE/Buerger/Migration-Integration/Spaetaussiedler/Statistik/Zeitreihe_1992_2016_SES.pdf [17. August 2017]

Evangelische Kirche in Deutschland (EKD) (2009):
„... denn ihr seid selbst Fremde gewesen.“
Vielfalt anerkennen und gestalten.

EKD Text 108, Hannover

Evangelische Kirche in Deutschland (EKD) (2017):
„... und ihr habt mich aufgenommen.“

Zehn Überzeugungen zu Flucht und Integration aus evangelischer Sicht.

URL: www.ekd.de/ekd_de/ds_doc/2017-04-11_Wort_zur_Lage.PDF

Gemeinsam evangelisch. Erfahrungen, theologische Orientierungen und Perspektiven für die Arbeit mit Gemeinden anderer Sprache und Herkunft.

EKD Text 119, Hannover 2014.

URL: www.ekd.de/Gemeinsam-evangelisch-1091.htm

Deutsche Hugenotten-Gesellschaft e. V. (2017):
Geschichte der Hugenotten.

URL: www.hugenotten.de/hugenotten/geschichte.php [17. Juli 2017]

Die Bundesregierung (o.J.): **Flucht und Asyl: Fakten und Hintergründe.**

URL: <https://www.bundesregierung.de/breg-de/themen/flucht-und-asyl> [8. August 2017]

Gatrell, Peter (2016):

60 Jahre Genfer Flüchtlingskonvention.

In: Bundeszentrale für politische Bildung (Hrsg.): Aus Politik und Zeitgeschichte (26/27–2016). Flucht historisch. Bonn, Seiten 25–32

Hamann, Ulrike / Karakayali, Serhat / Höfler, Leif Jannis / Lambert, Laura / Meyer, Leoni (2017): **Pionierinnen der Willkommenskultur.** Strukturen und Motive des Engagements für Geflüchtete.

In: Berliner Institut für empirische Integrations- und Migrationsforschung (Hrsg.): Forschungsbericht. Forschungs-Interventions-Cluster „Solidarität im Wandel?“. Humboldt-Universität zu Berlin, Seiten 102–118

Heidelberger Institut für internationale Konfliktforschung (2016):
Conflict-Barometer 2015

Hirsch, Thomas / Schalke, Ingrid (2009):
Auswirkungen der Wirtschafts-, Klima- und Ernährungskrise auf extrem Arme.

In: Social Watch Deutschland (Hrsg.): Globale Krisen. Soziale Auswirkungen – politische Konsequenzen. Ein internationaler Bericht zivilgesellschaftlicher Organisationen über den Fortschritt bei der Armutsbekämpfung und Gleichstellung der Geschlechter. Montevideo

Institut für Kirche und Gesellschaft der Evangelischen Kirche von Westfalen:
Was Engagierte bewegt. Ergebnisse einer Befragung von Engagierten in der Flüchtlingsarbeit (2018)

URL: www.kircheundgesellschaft.de/fileadmin/Dateien/Das_Institut/FMI_Engagiert-in-Vielfalt/181010_Broschuere_Engagiert_in_Vielfalt_-_Was_Engagierte_bewegt.pdf

Kahl, Werner: **Vom Verweben des Eigenen mit dem Fremden.** Impulse zu einer transkulturellen Neuformierung des evangelischen Gemeindelebens. Studien zu interkultureller Theologie an der Missionsakademie

Missionshilfeverlag Hamburg 2016, URL: http://www.missionsakademie.de/de/pdf/sitma_9.pdf

Koopmann, Ruud (2017):
Assimilation oder Multikulturalismus?
Bedingungen gelungener Integration

Kühn, Heinz (1979):
Stand und Weiterentwicklung der Integration der ausländischen Arbeitnehmer und ihrer Familien in der Bundesrepublik Deutschland: Memorandum der Beauftragten der Bundesregierung.

Bundesminister für Arbeit und Sozialordnung, Bonn. URL: www.migration-online.de/data/khnmemorandum_1.pdf [17. Juli 2017]

Ministerium für Arbeit, Integration und Soziales des Landes Nordrhein-Westfalen (2016a):
Teilhabe- und Integrationsbericht Nordrhein-Westfalen.

1. Bericht nach § 15 des Teilhabe- und Integrationsgesetzes, Düsseldorf.

URL: www.integrationsmonitoring.nrw.de/integrationsberichterstattung_nrw/berichte_analysen/Zuwanderungs-_und_Integrationsberichte/index.php [17. Juli 2017]

Nagel, Alexander K./El-Menouar, Yasemin (2017):
Engagement für Geflüchtete – eine Sache des Glaubens?

Die Rolle der Religion für die Flüchtlingshilfe.

Bertelsmann Stiftung, Gütersloh. URL: https://www.bertelsmann-stiftung.de/fileadmin/files/Projekte/51_Religionsmonitor/BSt_ReligionsmonitorFluechtlingshilfe_3_2017_web.pdf [11. Juli 2017]

PRO ASYL (2017): **EU-Asylpolitik. Ein Überblick.**

URL: www.proasyl.de/thema/eu-asylpolitik/ [19. Juli 2017]

PRO ASYL, Diakonie Deutschland, u. a. (2013):
Memorandum Flüchtlingsaufnahme in der Europäischen Union: Für ein gerechtes und solidarisches System der Verantwortlichkeit.

URL: www.proasyl.de/wp-content/uploads/2015/12/PRO__ASYL_Memorandum_Dublin_deutsch_Maerz_2013-1.pdf

PRO ASYL, Diakonie Deutschland, u. a. (2016):
Memorandum für faire und sorgfältige Asylverfahren in Deutschland. Standards zur Gewährleistung der asylrechtlichen Verfahrensgarantien.

URL: www.proasyl.de/wp-content/uploads/2016/11/PRO__ASYL_Memorandum_BAMF_Broschuere_Web_Nov16.pdf

Sachverständigenrat Deutscher Stiftungen für Migration (2018): **Steuern, was zu steuern ist: was können Einwanderungs- und Integrationsgesetze leisten?** Jahresgutachten 2018

Osnabrück

Schäfer, Gerhard (Hrsg.), u. a. (2016):
Geflüchtete in Deutschland.
Ansichten – Allianzen – Anstöße

Statistisches Bundesamt (2017): **Bevölkerung und Erwerbstätigkeit. Ausländische Bevölkerung.** Ergebnisse des Ausländerzentralregisters 2016.

Fachserie 1, Reihe 2. URL: www.destatis.de/DE/Publikationen/Thematisch/Bevoelkerung/MigrationIntegration/AuslaendBevoelkerung2010200167004.pdf?__blob=publicationFile [22. Juli 2017]

Südwind e.V. – Institut für Ökonomie und Ökumene (2017): **Migration und Flucht in Zeiten der Globalisierung.**

Die Zusammenhänge zwischen Migration, globaler Ungleichheit und Entwicklung

Bonn

„... und der Fremdling, der in deinen Toren ist.“

Gemeinsames Wort der Kirchen zu den Herausforderungen durch Migration und Flucht (1997)

Bonn/Frankfurt am Main/Hannover

Von Vieregge, Henning (2017):
Vertrauensbildung und Beheimatung. Flüchtlingshilfe als Chance für Kirchengemeinden

Deutsches Pfarrerverband 5/17. URL: www.pfarrerverband.de/pfarrerverband/archiv.php?a=show&id=4282 [31. Juli 2017]

Wegner, Gerhard (2016):
Religiöse Kommunikation und soziales Engagement. Die Zukunft des liberalen Paradigmas.

Leipzig



